Nipashe
Alhamisi Novemba 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581874
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
Nipashe digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

UCHAGUZI S/MITAA...

# Kura zapigwa, dosari zashtua

• **Samia** ataka washindi watangazwe, mgombea auawa kwa risasi, nyumba ya mbunge yanusurika kuchomwa... *Endelea Ukurasa 2 & 3*



Rais Samia Suluhu Hassan akipiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mtaa katika kitongoji cha Sokoine, Chamwino mkoani Dodoma jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe akipiga kura jimboni Hai na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu jimboni Tunduru.

# Ndugulile afariki dunia kabla kukalia kiti chake kipya WHO

• **Rais**, UN, vyama vya siasa, spika waguswa... *Endelea Ukurasa 4*



MICHEZO RAMOVIC: WACHEZAJI WANGU HAWAKO FITI UK.24 MAONI, UK.6

# Kura zapigwa, dosari zashtua

**Na Waandishi Wetu**

UPIGAJI kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika jana, ulikwenda vizuri katika maeneo mengi huku baadhi ya maeneo ukikumbwa na kasoro zilizotia doa mchakato huo.

Huku upigaji kura ukifanyika kwa namna hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza matokeo yatakayotangazwa ni yale ya kura zilizohesabiwa kwenye masanduku ya kura na si vinginevyo.

**AGIZO LA SAMIA**

Akizungumza jana baada ya kupiga kura katika Kituo cha Sokoine, Kijiji cha Chamwino, Ikulu mkoani Dodoma, Rais Samia aliagiza kuwa matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa yatolewe kwa mujibu wa kura zilizopigwa kwenye masanduku ya kura.

"Watanzania wakapige kura kwa maelewano na masanduku ya kura yanavyosema ndivyo matokeo yatoke. Nimeona watu ni wengi wamejitokeza na kura hizi ni mtindo wa demokrasia na utamaduni wetu wa kisiasa. Waende kuufanya kwa usalama na kwa amani. Wasivunje amani yetu," alisema.

**WALIOUAWA**

Viongozi wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefariki dunia akiwamo mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji cha Stendi, Kata ya Mkwese wilayani Manyoni, George Mohamed (41).

Pia Katibu wa CHADEMA, Jimbo la Singida Mjini, Hamis Nkua, amechomwa kisu kwenye bega akiwa Kata ya Mandewa na watu wanaodhaniwa ni makada wa chama (jina limehifadhiwa) kisha akakimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida.

Jana, Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida lilisema linamshikilia Askari wa Jeshi Magereza kwa tuhuma za kusababisha mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari alisema tukio hilo la mauaji hayo lilitokea Novemba 25, mwaka huu, saa 5:00 usiku katika Kitongoji cha Stendi Kata ya Mkwese wilayani Manyoni.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni kwamba katika eneo la tukio, wafuasi wa CCM walikuwa katika nyumba moja wakifanya kikao cha ndani na ghafla walivamiwa na wafuasi wa CHADEMA, hivyo kusababisha vurugu.

Kamanda Kakwale alisema kutokana na vurugu hizo, askari magereza ambao wako eneo la Magereza walipigiwa simu kuhusu vurugu hizo na ikabidi waende kuona hali ilivyo huku wakiwasiliana na polisi.

Alisema askari walipofika eneo la tukio, walianza kushambuliwa kwa mawe jambo lililowalazimu kupiga risasi hewani kuwahadharisha na kuwazuia watu waliokuwa wakiwashambulia kwa mawe.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Manyoni, Danny Butale, akizungumza na Nipashe jana kwa simu akiwa njiani kwenda Tarime mkoani Mara, alisema tukio hilo lilitokea saa 7:00 usiku. Alisema mwili wa Juma ulipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni baada ya kuuawa.

Alisema kabla ya tukio kutokea, magari mawili yalifika usiku nyumbani kwa mgombea huyo na kuvamia kisha kumpiga risasi kiunoni na kupoteza maisha papo hapo.

Mkoani Songwe, kiongozi wa CHADEMA Jimbo la Tunduma, Steven Chalamila, alivamiwa nyumbani na kukatwakatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake na kufariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Augustino Senga, alithibitisha kifo cha Stephano Mwambeje (23) mkazi wa Chawa A Wilaya ya Momba kuwa alivamiwa na watu wasiojulikana na kukatwakatwa na kitu chenye kali kichwani na mikononi, hivyo kusababisha kifo chake.

Senga alisema Mwambeje alivamiwa usiku wa kuamkia jana majira ya saa 4:30 akiwa nyumbani kwake amelala baada ya watuhumiwa kuvunja mlango.

Alisema hadi sasa Jeshi la Polisi limemkamata mwanamume, dereva wa bodaboda kwa mahojiano ili kufahamu chanzo cha tukio hilo na wengine waliohusika ni kina nani.

**JARIBIO KUCHOMA NYUMBA**

Mkoani Rukwa, vijana waliovalia sare za chama kimoja cha siasa, wanadaiwa kuvamia nyumbani kwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, wakitaka kuchoma nyumba yake.

Khenani alisema vijana hao walikuwa wamebeba dumu lenye mafuta ya petroli na walidhibitiwa na wanachama wa CHADEMA waliokuwapo nyumbani kwake.

Inadaiwa tukio hilo lilitokea saa 4:00 usiku na kwamba pamoja na kuwa kwenye sare hizo hizo, pia walikuwa wakitumia pikipiki inayodaiwa ni mali ya chama hicho (kimehifadhiwa) yenye usajili Namba MC 992 EHY.

"Unajua hapa nyumbani pamoja na kuwa na familia yangu kwa maana ya mume wangu, pia walikuwapo baadhi ya mawakala na wagombea wengine wa CHADEMA wanaogombea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Tulikuwa tukiendelea na mazungumzo yetu ghafla tukasikia watu wakizunguka nyumba ndipo tulipojipanga na kufanikiwa kuwakamata," alisema.



Polisi wakiwadhibiti vijana waliokuwa wanapigana wakituhumiana kuweka kura feki kituo cha Shule ya Msingi Kibirizi, mjini Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Kwa mujibu wa Khenani, baada ya kuwakamata vijana hao na kuwahoji, walidai kuwa walitumwa na kiongozi mmoja wa juu wa serikali ngazi ya wilaya kwa nia ya kuiteketeza nyumba hiyo pasipo kujali ndani atakuwapo kina nani kwa kuwa yeye ndiye mlengwa mkuu.

Khenani alisema baada ya mahojiano na vijana hao waliokuwa wakiomba wasiuawe, alitoa taarifa polisi ambao walifika eneo la tukio na kuwakamata na kwenda kuwahoji na bado wanashikiliwa na polisi wilayani Nkasi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Shadrack Masija, alikiri kupata taarifa ya tukio hilo na kusisitiza atatoa taarifa yake kwa vyombo vya habari.

**MAJINA KUKOSEKANA**

Katika baadhi ya maeneo kulijitokeza kasoro kadhaa ikiwamo majina ya wapigakura kutokuonekana, hivyo kushindwa kupiga kura.

Baadhi ya maeneo hayo ni Tabata Liwiti na Shule ya Sekondari Migombani ambako majina ya wananchi hao, licha ya kujiandikisha, hayakuonekana katika sehemu zilizobandikwa.

Katika Kata ya Liwiti, mwandishi alishuhudia wananchi watano, akiwamo Joachim Mhagama kutoka kituo cha Zahanati ya NBC waliofika kupiga kura, lakini wakarudi nyumbani kwa shingo upande baada ya kutoona majina yao.

"Nimefika hapa kutimiza haki yangu ya kupiga kura lakini ndio hivyo nalazimika kurudi nyumbani kwa sababu jina langu halipo kwenye orodha ya waliojiandikisha," alisema.

Mmoja wa wapigakura katika kituo cha Misewe, Ally Salehe, alimweleza mwandishi kuwa ametafuta jina lake kwa dakika 15 bila mafanikio, hivyo hakuona haja ya kuendelea kusubiri.

Katika kituo cha Segerea, uchaguzi wa Mtaa wa Migombani, uligubikwa na kasoro kadhaa zikiwamo wananchi kutokuona majina yao, watu kuingia kupiga kura bila kuona majina na kutokuhakikiwa kama ni watu sahihi kwa maana ya kukaguliwa vitambulisho vyao.

**MCHEZO MCHAFU**

Madai ya kuwapo vitendo vinavyoashiria kuwapo kwa ukiukwaji wa upigaji kura pia vilijitokeza.

Katika kituo cha Zahanati ya NBC, Liwiti, viongozi wa CHADEMA walikilalamikia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kufanya vitendo kinyume cha sheria za uchaguzi, ikiwamo kuingiza wapigakura katika ofisi zao na baadaye kwenda kwenye eneo la kupiga kura.

Katibu wa CHADEMA Kata ya Liwiti, Stanley Mmanyi, alisema si sahihi wapigakura kuingia katika ofisi za CCM kwanza kisha kupiga kura kwa kuwa inaleta taswira ya kuibiwa kura.

Alisema anahisi walioingia katika ofisi hiyo sio watu wa mtaa huo bali wanakwenda kupewa majina ya watu hewa walioandikishwa ili watumie kupiga kura.

Alisema pia walikamata baadhi ya wagombea wa CCM, akiwamo anayegombea ujumbe wa serikali ya mtaa, Mussa Mwinjuma, wakibandika mabango ya kampeni jana asubuhi jambo ambalo ni kinyume na sheria za uchaguzi.

"Hata katika Mtaa wa Mfaume, leo asubuhi (jana) mtoto wa mgombea wa nafasi ya uenyekiti amekutwa akifanya kampeni nyumba kwa nyumba kuhamasisha watu wakampigie kura baba yake," alisema.

Aidha, kulikuwa na malumbano kati ya mgombea wa Uenyekiti Serikali ya Mitaa (CHADEMA), James Joseph, na msimamizi katika kituo hicho baada ya kutumia simu kufanya mawasiliano kinyume na sheria za uchaguzi.

Katika Kituo cha Liwiti, vitabu vya kupigia kura vilivyotumika awali vilikuwa vya kituo kingine, jambo lililogunduliwa na mgombea ujumbe kundi mchanganyiko kupitia tiketi ya CHADEMA, Oscar Njau, na kuutarifu uongozi na wakabadilisha vitabu hivyo.

Kasoro kama hizo pia zilijitokeza katika Kata ya Sokoni One, Arusha, baada ya baadhi ya wananchi kushindwa kupiga kura kutokana na majina yao kutokuwapo kwenye daftari.

Wananchi hao waliiambia Nipashe kuwa walijitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari kwenye kituo cha Logdong Kata ya Sokoni One lakini cha kushangaza jana majina yao hayakuwapo na waliyoyakuta ni ya watu wengine kabisa.

Katika Kituo cha Engasengiu, Kata ya Sinoni, mgombea wa nafasi ya mwenyekiti, Damiano Mollel (CHADEMA), aliangua kilio baada ya kukosa jina lake kwenye kituo cha kura, kitu ambacho alidai ni hujuma zimefanyika dhidi yake.

**MAWAKALA WAZUIWA**

Baadhi ya maeneo jijini Arusha, kumekuwa na mvurugano na sitofahamu kutokana na mawakala wa vyama vya upinzani kutokuwapo katika vituo vya kupigia kura hasa Kata ya Unga Limited.

Akizungumzia hali hiyo, Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Arusha, John Kayombo, alisema vyama 12 vimechukua fomu na wasimamizi wao na kula kiapo isipokuwa CHADEMA pekee.

"CHADEMA waliweka mawakala wengi, yaani unakuta kituo kimoja mawakala watano au watatu kitu ambacho ni kinyume na utaratibu. Tuliwaita waje wapunguze baadhi ya mawakala na wabaki wale wanaohitajika lakini hadi jana (juzi) jioni walikuwa bado wana mvutano na hakuna hadi sasa waliokula kiapo," alisema Kayombo.

Aidha, katika Mtaa wa Nado Kati, Kata ya Muriet, masanduku ya kupigia kura yalichelewa kufika hadi saa 4:00 asubuhi. Katika Mtaa wa Muriet Mashariki, masanduku ya kura yalifika majira ya saa 09:30 asubuhi.

Kutokana na kasoro hizo, mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Makongoro, Albert Makingile (CCM), alishauri kuwa kuna haja serikali kutoa namba kwa kila raia, ambazo zitawezesha kutambua jina lake kwa haraka.

**MWAMKO MDOGO**

Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, alisema mwamko mdogo wa vijana katika upigaji wa kura umechangiwa na baadhi yao kutotulia mahali pamoja kutokana na shughuli za utafutaji.

Mkoani Tanga, Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah Issa, baada ya kupiga kura katika Ofisi ya Mtendaji Kata ya Mbaramo, aliwasihi wananchi wapige kura mapema na wasibubiri dakika za lala salama.

**•Imeandikwa na Godfrey Mushi, Cynthia Mwilolezi (Arusha), Mary Mosha (Moshi), Oscar Assenga (Tanga), Mussa Mwangoka (Katavi), Jenipher Gilla (DAR) na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA).**

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***

UCHAGUZI S/MITAA

# Dosari zaripotiwa Uchaguzi Serikali za Mitaa

Na Waandishi Wetu

MALALAMIKO ya kasoro katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yametolewa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama cha ACT-Wazalendo, huku baadhi ya wapigakura wakiamua kulinda kura.

Vyama hivyo vimetafsiri kasoro hizo kuwa ni hujuma kwa kuwa wagombea pamoja na mawakala wao wanadaiwa kukamatwa vituoni na katika maeneo mengine kuchelewa kuanza upigaji kura kwa madai ya kuchelewa karatasi za kura au kuchanganya vitabu vyenye orodha ya wapigakura, vingine kupelekwa kituo A au B.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alidai jana kuwa katika maeneo ya Chato, mjini Bariadi, mjini Kibaha, Msalala na Igunga, karatasi zilizokwisha kupigwa kura zilikamatwa.

"Katika eneo la Chato, karatasi za kura zilikamatwa kata ya Nyaruntembo, kijiji cha Nyantimba, kituo cha kupigia kura Nyantimba maboksi yenye kura ambazo zimeshapigwa tayari yamekamatwa kituoni na wananchi. Polisi wamefika na kuwakamata viongozi wetu na wameondoka na maboksi hayo yenye kura.

"Bariadi, kata ya Malambo, mtaa wa Nyashanda, zimekamatwa kura ambazo tayari zilishapigwa," alidai Mrema na kuongeza kuwa katika maeneo ya Msalala, kata ya Bugarama, kijiji cha Igudija, mpaka saa nne asubuhi jana upigaji kura ulikuwa haujaanza.

"Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Pwani, Bumija Senkondo amekamatwa, yuko ndani. Katika Jimbo la Segerea, kata ya Kisukuru, mtaa wa Kuhanga, karatasi za kupigia kura zimepelekwa mtaa wa Chanika, jimbo la Ukonga, Daftari la Wakazi lililopo kituoni hapo ni la mtaa wa Mainzini badala ya Luhanga, polisi wameitwa na wapo kwenye kituo hicho," alidai.

Alisema chama hicho kimeitaka Ofisi ya Rais - TAMISEMI itoe maelezo kwa umma kuhusu kura ambazo zilikamatwa tayari zimeshapigwa kwa wagombea maeneo mbalimbali ya nchi na hatua ambazo imepanga kuchukua dhidi ya wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo hayo.

Makamu Mwenyekiti wa ACT - Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita, alisema uchaguzi umekumbwa na changamoto kubwa zinazotilia shaka uhalali wa mchakato huo.

Akizungumza baada ya kupiga kura katika mtaa wa Likotwa, mkoani Lindi, Mchinjita alitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na ukamataji kura feki, kuondolewa mawakala wa chama hicho kwenye vituo vya kupigia kura na kutokuwapo majina ya baadhi ya wagombea kwenye karatasi za kura.

Kiongozi mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema uchaguzi huo ni fursa kwa wananchi kupata viongozi wa karibu wanaoshughulikia changamoto za moja kwa moja katika maeneo yao.

Zitto alisema ushiriki wa kila raia ni muhimu katika kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unafanikiwa kwa haki na uwazi.

**MATUKIO**

Katika baadhi ya maeneo nchini, kumeripotiwa matukio yasiyo ya kawaida, ikiwamo baadhi ya wakazi kutoona majina yao, wasimamizi wa uchaguzi kutowasili kwa wakati vituoni, madai ya kuwapo kura feki na makada wa CHADEMA kuuawa.

Katika jimbo la Mikumi, wilayani Kilosa, kata saba zilichelewa kupiga kura kwa saa 2:30, kwa kile kilichoelezwa ni kuchelewa karatasi za kupigakura za wajumbe mchanganyiko wa serikali za vijiji na za wajumbe wa serikali za vijiji kundi la wanawake.

Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Mikumi, Ally Rashid, alisema jana kuwa hadi saa 4:30 asubuhi, kata zilizokuwa hazijaanza upigaji kura ni Ruaha, Ruhembe, Mabwerebwere, Masanze, Zombo, Tindiga na Kidodi.

Alidai kata tatu za Kilangali, Ulaya na Mhenda zilisimama kuendelea na uchaguzi kwa kile kilichoelezwa ni kuisha kwa karatasi za kupigia kura.

Katika Manispaa ya Musoma, mkoani Mara, wakazi wa vituo tofauti waliripotiwa kushindwa kupigakura baada ya kukuta majina yao hayasomeki vizuri, hali iliyowakatisha tamaa wengine na kulazimika kuondoka vituoni.

Mjini Tunduma, wilayani Momba, mkoani Songwe, kada wa CHADEMA, Steven Chalamila, aliripotiwa kushambuliwa kwa mapanga na kuuawa baada ya kuvamiwa nyumbani kwake, usiku wa kuamkia jana.

Jijini Mwanza, Mkurugenzi wa Jiji, Kiomoni Kibamba, alidai kuwa baadhi ya vijana katika kata ya Lwahnima, walivamia kituo cha kupigia kura za mwenyekiti na kutoweka nazo. Jitihada zilifanywa na watu hao walikamatwa.

Katika mtaa wa Sinza B, kata ya Sinza, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, wakazi wa eneo hilo walilalamikia kuchelewa kubandikwa kwa majina yao nje ya kituo cha kupiga kura cha Shule ya Sekondari Mashujaa na baada ya kulalamika, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi walianza kuyabandika.

Mkoani Dodoma, iliripotiwa kuwa baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi walichelewa kufika vituoni, vikiwamo vya Ofisi ya Kata ya Chamwino na cha Nduka.

Mkoani Kigoma, mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mgera B, kata ya Mwandiga (CCM), Safiania Barikure,



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji Jacobs Mwambegele, akipiga kura katika kituo cha Shule ya Sekondari Jamhuri kilichoko Halmashari ya Jiji la Ilala, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: INEC**

alikamatwa jana alfajiri kwa madai ya kukutwa na kura ambazo zilikuwa na mhuri wa Tume ya Uchaguzi.

Katika kituo cha Mlimwa, Dodoma, kuliibua mvutano kati ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Aisha Madoga na wasimamizi wa uchaguzi baada ya kubainika kuna mwananchi ambaye si mpigakura wa eneo hilo, amepiga kura bila kuonesha kielezo wala kuangaliwa katika daftari.

Madoga alipobaini hali hiyo alitishia kuondoka na daftari la wapigakura, lakini askari aliyekuwapo kituoni aliingilia kati na kumzuia.

"Nimekuja hapa na rafiki yangu ambaye si mkazi wa eneo hilo na hajajiandikisha kupiga kura katika mtaa huu, lakini cha kushangaza ameruhusiwa kupiga kura, huu si utaratibu uliowekwa, wanapaswa wasimamizi katika vituo waangalie majina ya watu kama yapo ndipo waruhusiwe kupiga kura," alisema Madoga .

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo mkoani Dodoma, Yohana Mussa alilalamikia mawakala wao kuzuiliwa kwa muda kuingia katika kituo cha kupigia kura Mtaa wa Mbuyuni, kata ya Kizota. Badala ya kuingia saa mbili asubuhi walidai kuruhusiwa kuingia saa tano asubuhi.

Msimamizi wa Uchaguzi Jiji la Dodoma, Dk. Fredrick Sagamiko, aliahidi kutoa ufafanuzi baadaye kwa madai kuwa alikuwa anazunguka vituoni kuangalia kinachojiri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi alipoulizwa kama kuna watu wanashikiliwa kuhusiana na uchaguzi huo, alisema hali ya uchaguzi ni shwari na suala la kura bandia hakuwa na taarifa nalo, akiahidi kufuatilia.

Mkoani Arusha, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa alidai chama hicho hakijatendwa haki katika baadhi ya maeneo, kwa kuwa mawakala wao walinyimwa nafasi ya kusimamia kwa muda mwafaka, badala yake walicheleweshwa kuanza kusimamia upigaji kura.

"Rafu ni nyingi tulizofanyiwa na Msimamizi wa Uchaguzi, sasa hatuelewi wanataka nani ashinde, wakati tunasema uchaguzi ni demokrasia, kwanini hatutendwi haki vyama vingine kama CHADEMA?" alihoji.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Murtallah Mbillu, alikanusha taarifa iliyosambazwa katika mitandao ya kijamii kwamba polisi walisindikiza masanduku ya kura zilizopigwa wilayani humo.

"Taarifa sahihi ni kwamba wakala wa CHADEMA ambaye alitakiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura cha Ndoinyo, kijiji cha Nasiporion, kata ya Endulen, tarafa ya Ngorongoro, alitakiwa kuwa katika kituo hicho saa mbili asubuhi, wakati wa kufungua kituo, yeye alifika akiwa amechelewa bila taarifa yoyote.

"Kwa vile muda wa kufungua kituo ili wananchi waanze kupiga kura ulishafika, upigaji kura ulianza. Alipofika ndipo akaanza kupiga picha na kuzituma anakofahamu yeye na waliotumiwa wakatengeneza taarifa hiyo ya uongo, wakiwa na lengo wanalolijua wao," alidai.

Baadhi ya wafuasi wa CHADEMA Kata ya Chamwino, jijini Dodoma walisema kuwa pamoja na kumaliza kupiga kura, hawataondoka vituoni, bali wataendelea kubaki ili kulinda kura zao.

Mmoja wa wafuasi wa chama hicho, Kombo Adam, akiwa katika kituo cha mtaa wa Mailimbili, alisema wamekubaliana kutoondoka eneo hilo hadi matokeo yatakapotangazwa.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama Wakulima (AAFP), Marck Mhomela, alilalamikia kitendo cha baadhi ya mawakala wao kuzuiwa kuingia katika vituo vya uchaguzi.

Alidai kuwa katika kata ya Makole, jijini Dodoma, mmoja wa mawakala wao alikataliwa kuingia kituoni, hali iliyowalazimu kutumia nguvu ya ziada kupata kibali cha kuingia.

Mkoani Pwani, Mwenyekiti wa CHADEMA mkoani humo, Bumija Moses pamoja na wakala wa chama hicho katika mtaa wa Mkongoni walishindwa kupiga kura baada ya kushikiliwa na polisi kwa saa sita, wakidaiwa kumfanyia fujo msimamizi wa uchaguzi.

Akizungumza baada ya kuachiwa kwa dhamana, mwenyekiti huyo alisema wakiwa katika kituo cha Mkongoni, msimamizi wa kituo alionekana akiwa na masanduku matatu yakiwa na kura ambazo tayari zimepigwa.

Alisema wananchi waliokuwa kituoni, walishangazwa na jambo hilo, hivyo walimpigia simu ili afike kufuatilia suala hilo na wakati anafuatilia ndipo alipoambiwa anafanya fujo na kupelekwa polisi akiwa na wakala wa CCM na CHADEMA.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase, alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kufanya fujo kwa madai ya kutokuwa na imani na msimamizi wa kituo cha Mkongoni Kibaha.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini walilenga kuharibu uchaguzi na kuleta taharuki kwa jamii.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Sabato Kasika (DAR), Paul Mabeja na Peter Mkwavila (DODOMA), Idda Mushi (Morogoro) na Julieth Mkireri (KIBAHA)**

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Ndugulile afariki dunia kabla kukalia kiti chake kipya WHO

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Kigamboni ambaye pia ni Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, Dk. Faustine Ndugulile, amefariki dunia India alikokuwa anapatiwa matibabu.

Rais Samia Suluhu Hassan, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, WHO na wadau kwa nyakati tofauti jana, walieleza masikitiko yao kumpoteza kiongozi huyo ambaye amekuwa na mchango mkubwa katika sekta mbalimbali, ikiwamo afya.

Rais Samia alisema, "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Dk. Ndugulile, na kutoa salamu za pole kwa familia, Spika wa Bunge, wabunge, wananchi wa Kigamboni, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wote.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia alisema kifo cha Dk. Ndugulile kilichotokea usiku wa kuamkia jana, kimeacha simanzi kubwa kwa Bunge na watanzania kwa ujumla kutokana na mchango wake mkubwa katika maendeleo ya taifa.

Akizungumza jana mara baada ya kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, huko mtaa wa Uzunguni A, jijini Mbeya, Spika Tulia alisema nyota ya Dk. Ndugulile imezimika wakati akiwa ameanza kung'ara katika anga za kimataifa.

"Misiba yote ni migumu lakini kwa msiba huu ni mgumu zaidi kwa sababu pamoja na kwamba alikuwa mbunge, alikuwa mtu ambaye dunia imeshamwamini, ukiacha nafasi mbalimbali hapa nchini alizowahi kuzifanyia kazi.

"Alikuwa ameshaaminiwa kutuwakilisha kuwa Mkurugenzi mkubwa WHO Kanda ya Afrika. Wote tulishiriki kwa maombi na Mheshimiwa Rais alishiriki kwa maombi kuhakikisha nafasi hii inakuja Tanzania, sasa mipango ya mwanadamu na Mungu ni tofauti," alisema.

Dk. Tulia alisema Dk. Ndugulile pia ametoa mchango katika eneo la afya na kwa kipindi hiki alikuwa Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ambapo kuna sera zimebadilika na sheria zimetungwa kwa sababu ya michango yake.

"Mimi ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kule nako alikuwa anaongoza kundi linaloshughulikia masuala ya afya. Mchango wake katika sekta ya afya ni mkubwa, ni mmoja wa viongozi ambao tumewapoteza kipindi ambacho tunawahitaji zaidi," alisema Dk. Tulia.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma, Ofisi ya Bunge, ilisema Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia wanaendelea kuratibu shughuli za mazishi na taarifa zaidi zitatolewa.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO), Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus kupitia mtandao wa X jana aliandika:

"Nimeshtushwa na kusikitishwa sana na taarifa za msiba wa ghafla wa Dk. Faustine Ndugulile, Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (Kanda ya Afrika), Salamu zangu za rambirambi kwa familia, Bunge na wananchi wa Tanzania."

**CCM YAMLILIA**

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, alisema wameshtushwa kwa sababu Dk. Ndugulile alikuwa akiwakilisha Tanzania duniani.

"Alikuwa kada wa CCM na mwanachama mwaminifu, ametumikia unaibu waziri na uwaziri. Ni pigo kubwa kwa Tanzania na dunia aliyokuwa anakwenda kwenye nafasi ya Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, tumepoteza mtu makini na mwenye weledi, mzalendo. CCM inamlilia," alisema.

Makalla ambaye pia ni Mlezi wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema, Dk. Ndugulile ametoka Tanzania akiwa bado ni mbunge, alikuwa anapenda wananchi wake na alikuwa kiongozi mfuatiliaji.

Godbless Lema, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, alisema jana kuwa, "maisha haya tunapita haraka kama upepo. Kuishi kwa mema ni jukumu la msingi kabisa katika maisha.

"Hata sijui kwa nini binadamu tunakuwa na viburi. Nilimfahamu Dk. Ndugulile tukiwa bungeni. Nimeshtuka kusikia amefariki dunia, jipeni moyo sana familia, ndugu, jamaa na marafiki."

**KAULI YAKE BUNGENI**

Septemba 3 mwaka huu, wakati akitoa shukrani bungeni, Dodoma, Dk. Ndugulile alisema: "Niwaombe mniombee, tuendeleze sala na dua nyingi, kwani nafasi hii imebeba maono ya watanzania na waafrika wanatarajia makubwa."



**"Alikuwa ameshaaminiwa kutuwakilisha kuwa Mkurugenzi mkubwa WHO Kanda ya Afrika. Wote tulishiriki kwa maombi na Mheshimiwa Rais alishiriki kwa maombi kuhakikisha nafasi hii inakuja Tanzania, sasa mipango ya mwanadamu na Mungu ni tofauti," alisema.**

Dk. Ndugulile ni mtanzania wa kwanza na mwana Afrika Mashariki wa kwanza kuteuliwa kushika nafasi hiyo nyeti WHO. Na kituo chake cha kazi kilikuwa ni Congo Brazzavile.

Machi 27 mwaka huu, alipata ushindi huo baada ya nchi 19 kuipigia kura Tanzania katika mzunguko wa kwanza, 12 wakiipigia Senegal, saba Niger na nchi saba zikiipigia Rwanda. Matokeo yalitangazwa siku hiyo katika Mkutano wa Afya wa 78 wa WHO uliofanyika Congo Brazzaville.

Katika mzunguko wa pili wa uchaguzi, alipata kura 25, Senegal 14 na Niger kura sita. Dk. Ndugulile alipigiwa kura na mawaziri wa afya kutoka nchi za Afrika.

Machi 11, 2023, aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Ushauri Masuala ya Afya ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), akiwa sehemu ya wabunge 12 wanaoshauri IPU masuala ya afya, uteuzi ulioanza Februari mwaka huo.

Nafasi nyingine ambazo amewahi kuhudumu ni pamoja na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Uchunguzi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (2004-2006), Waziri wa Mawasiliano na Tekonolijia ya Habari (2020-2021) na Naibu Waziri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (2017-2020).

Mwaka 1997-1998, Dk. Ndugulile alikuwa daktari katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na alikuwa mtaalamu wa maikrobaiolojia hadi mwaka 2004 alipoteuliwa kuwa Meneja wa Programu Wizara ya Afya.

Mwaka 2004-2006, alihudumu kama Mkuu wa Kitengo cha Uchunguzi wizarani huko na mwaka 2007-2010 alikuwa Mshauri wa Afya katika Taasisi ya Udhibiti wa Magonjwa (CDC) Afrika Kusini. Kati ya mwaka 2006 na 2007 alihudumu kama Meneja Program katika Mpango wa Damu Salama.

**ELIMU**

Dk. Ndugulile alizaliwa Machi 31, 1969, wilayani Mbulu, mkoani Manyara. Alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Groombridge iliyoko Harare, Zimbabwe kuanzia mwaka 1976 na kuhitimu 1982.

Mwaka 1982-1986 alipata elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari Prince Edward, Harare na baada ya kufaulu, aliendelea na elimu ya kidato cha tano na sita katika Shule ya Tambaza iliyoko Dar es Salaam (mwaka 1987-1989).

Mwaka 1990-1997 alisomea shahada ya kwanza ya udaktari (MD) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na baadaye akachukua shahada ya uzamili (MMED) chuoni huko alikohitimu mwaka 2001.

Kukiwa na msiba huo wa kimataifa, Mchumi na Mwanataaluma Mbobezi, Dk. Oswald Mashindano, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana na msiba uko nyumbani kwake, Kijichi, Dar es Salaam.

Dk. Mashindano aliwahi kuwa Msajili wa Hazina, Mhadhiri Mwandamizi UDSM Idara ya Uchumi na Mtafiti Mwandamizi Mshiriki wa Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii (ESRF).

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz*



Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Sokoine Kijiji cha Chamwino Ikulu, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, wakiwa kwenye foleni ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mvua yapunguza kasi upigaji kura

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA baadhi ya mikoa ya Kanda ya Ziwa mvua iliyoanza kunyesha kuanzia majira ya saa 12:00 asubuhi hadi saa 6:30 mchana ilipunguza kasi ya upigaji kura kutokana na baadhi ya vituo watu kwenda mmoja mmoja tofauti na utaratibu wa kawaida wa kuwa na mistari.

Hadi mvua inakata mwandishi wa habari hii alishuhudia wapigakura wasiopungua 10 walioingia kituoni hapo.

Baadhi ya wapigakura waliofika kwa ajili ya kutekeleza haki yao ya kupiga kura akiwamo mkazi wa Majengo, Elizabeth Popa akizungumza na Nipashe baada ya kupiga kura alisema hakupata usumbufu wowote licha ya kuwa hali ya hewa kuwa ya mvua na kusababisha msongamano kutokuwa mkubwa.

"Mimi nimefika sasa hivi sijakuta foleni na nimepiga kura bila usumbufu nimeona jina langu na sasa naenda kwenye majukumu yangu," alisema Popa.

Naye Dotto Mathias alisema uchaguzi huu umefanyika kwa uhuru na haki na wasimamizi wanatoa maelekezo na unapiga kura bila kubugudhiwa hali ikiendelea hivyo mpaka jioni hatutakuwa na machafuko yoyote.

Kwa mujibu wa msimamizi wa kituo cha kupigia kura kilichopo Kata ya Bukandwe, Kijiji cha Ihayabuyaga, Magu, Mwanza, Valery Shigi, hadi kufikia majira ya saa sita walijitokeza wapiga kura wasiozidi 100.

Mkazi wa Mtaa wa Pwani, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Aline Ngw'aganugu, alisema, licha ya kuwa na mvua, ameweza kutoka ndani ili kutimiza haki ya kikatiba ya kuchagua kiongozi ambaye atakuwa msaada na mpigania wananchi wake.

Alisema katika kituo ambacho amepigia kura majina ya wapigakura yameonekana licha ya kuwa sio mengi zaidi sawa na vituo jirani ambavyo vina idadi kubwa ya wapigakura.

Mkazi wa Kahololo, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Joseph Alphonce, alisema katika ubao wa matangazo namba ya jina lake inatofautiana na iliyopo ndani katika jina la pili hali iliyosababisha utata awali, lakini baadaye akapiga kura na kuendelea na shughuli zake.

Mkazi wa Mtaa wa Uwanja wa Ndege wilayani Maswa, Simiyu, Phaustine Makeja, alisema kulikuwa na utaratibu mzuri na kuwa wasimamizi walikuwa wakisaidia kufanyika haraka licha ya mvua kunyesha, lakini hawakukutana na usumbufu wowote.

Diwani wa Kata ya Bukandwe, Marco Minzi, alisema wananchi wamejitokeza kwa wingi kuwapigia kura viongozi wao wanaowahitaji licha ya kuwapo na mvua zilizoanza kunyesha alfajiri hadi saa sita mchana huku akiwasihi wananchi kuendelea kujitokeza kupiga kura.

**VIONGOZI WANENA**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, akizungumza wakati wa kupiga kura katika Kituo cha Isamilo jijini Mwanza baada ya kubaini upungufu wa wapigakura aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupiga kura bila kujali mvua inayoendelea kunyesha.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, akizungumza baada ya kupiga kura kwenye kituo cha Pwani kilichopo Manispaa ya Bukoba mkoani humo aliwataka wananchi kuendelea kupiga kura kwa utulivu ili kukamilisha uchaguzi bila kuwapo kwa vurugu.

Alisema mkoa huo uko salama na wananchi wanaendelea kujitokeza kwa wingi katika vituo vyao kutimiza haki ya kupiga kura huku akiwaomba wananchi kuwa watulivu na kuzingatia taratibu za kupiga kura na wakimaliza warudi nyumbani kwao wapumzike wasubiri matokeo na asiwepo wakujaribu kufanya vurugu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema uchaguzi mkoani humo umefanyika kwa amani na utulivu, hakuna vurugu zozote kubwa ambazo zimefanyika za kuvuruga amani ya nchi

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, alisema upigaji kura unafanyika vyema na kuwa wananchi wameendelea kujitokeza kupiga kura na kuelekezwa cha kufanya pale wanapokwama hivyo kuwataka wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha wanaendelea kutoa ushirikiano ipasavyo kwa wapiga kura hao.

**WAKOSA MAJINA VITUONI**

Baadhi ya wananchi Joseph Peter Mkazi wa Manispaa ya Shinyanga wamelalamikia hatua ya kutobandikwa majina yao kwenye vituo vya kupigia kura, huku wengine wakidai kutoyaona na hivyo kushindwa kupiga kura.

Peter alisema katika kituo cha kupigia kura soko la Ndala Manispaa ya Shinyanga, alisema orodha ya majina ya wapigakura haikubandikwa kituoni hapo, hali ambayo iliwapa changamoto ya kuhakiki majina na hata kusababisha foleni kuwa ndefu.

Naye Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Serengeti, Jackson Mnyawami, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kuwa baadhi ya vituo ambavyo amevitembelea orodha ya majina ya wapigakura hayajabandikwa, na hivyo kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Estormine Henry, mkazi wa Mtaa wa Bugweto, alisema katika kituo chake cha kupigia kura hakuona jina lake, na kuamua kuondoka na kushindwa kupiga kura.

Mkazi wa wilayani Kahama, Zaria Kilimba alisema, licha ya kushiriki kikamilifu na kupata jina lake awali, lakini jana wakati wa kupiga kura alikosa jina hilo na kuondoka bila kupiga kura.

Msimamizi wa uchaguzi katika Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, akizungumzia suala la majina ya wananchi kutobandikwa kwenye baadhi ya vituo vya kupigia kura, alisema, kwenye vituo vya wazi ambavyo vipo 149 majina hayo hayajabandikwa kutokana na kuhofia mvua kulowesha makaratasi.

Alisema katika vituo hivyo vya wazi walichokifanya, daftari lenye orodha ya majina ya wapigakura, lilikuwa kwa wasimamizi wa uchaguzi kituoni na kila mtu kuhakikiwa jina lake na kushiriki kupiga kura.

Nipashe ilifanikiwa kuongea na baadhi ya wasimamizi wa vituo vya Nyasho Kati, Sido na Nyamatare, ambao walisema wananchi waliokosa majina yao kwenye ukuta wameyakuta kwenye daftari la kudumu la wapigakura na kuendelea kupiga kura.

**MGOMBEA MMOJA**

Mkazi wa wilayani Magu mkoani Mwanza, Emmanuel Mashauri, alisema hakwenda kupiga kura kutokana na eneo lake kuwa na mgombea mmoja na kuwa haoni haja ya kujisumbua kushinda kwenye kituo cha kupiga kura ili hali tayari mshindi anajulikana.

Naye Hawa Ramadhani Mkazi wa Mtaa wa Rwagasole jijini Mwanza alisema kuenguliwa kwa wagombea ambako kulilete sintofahamu kwa wananchi kumesababisha kutokuwa na hamasa ya kushiriki uchaguzi huo na kuamua kuendelea na shughuli za kibiashara.

**KAMPENI VITUONI**

Wananchi wa Kata ya Nyakato Mtaa wa Baruti, Kituo cha Sido Manispaa ya Musoma mkoani Mara, walilalamikia baadhi ya mawakala na wanachama wa vyama vya siasa kufanya kampeni za siri ndani ya vyumba vya kupigia kura wakiwalazimisha kupiga kura kwa vyama vyao.

Mpigakura Musira Aloyce alisema kuwa baadhi ya mawakala na wanachama kuwaelekeza wananchi kuchagua chama fulani bila wao kujua kuwa anayemhamasisha ni wa chama gani.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa gazeti hili ulibaini kuwapo kwa orodha ya majina yaliyobandikwa katika mbao za matangazo huku namba za majina zikiwa zimefunikwa na kusababisha wapigakura kuondoka bila kupiga kura na baadhi yao kuoneshwa majina yao kwenye daftari na kuelekezwa kuchagua chama.

Aidha, hali hii ilimfanya Mgombe wa nafasi ya ujumbe kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mtaa wa Nyahanga, Amri Mambo Kiboge, kushikiliwa na Jeshi la Polisi kwa muda baada ya kuonekana anapinga watu kuelekezwa namna ya kupiga kura huku wakiwa wanajua kusoma na kuandikwa.

Alisema, alitakiwa kuwekwa ndani kwa muda wa wiki mbili baada ya kutolewa amri na msimamizi wa uchaguzi, lakini amekuja kuachiwa mbele ya viongozi wake wa chama wilaya, kimkoa na kikanda waliopo kituo cha polisi Kahama.

Msimamizi wa uchaguzi wa mtaa wa Nyahanga, Elleni Mugenyi, alikiri baadhi ya wapigakura kukosa majina yako kwenye mbao za matangazo lakini kwenye daftari yalipatikana na kuhusu mgombea wa Chadema kukamatwa ni kweli kwasababu alikuwa kwenye chumba huku akiwa tayari ameshapiga kura.

Katibu Mwenezi wa CHADEMA Wilaya ya Kahama mkoani Shianyanga, Mustafa Kiyege, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kufanya vurugu kwenye kituo cha kupiga kura Mwime Machimboni wakati akizuia mawakala wa CCM aliodai kuingiza kura kwenye boksi zilizokuwa tayari zimepigwa.

Mwenyekiti wa chama hicho, Bukango Mussa aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari katika kituo cha kupiga kura cha Bukondamoyo Shuleni.

Jijini Mwanza wakati wa upigaji kura ukiendelea Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Jiji la Mwanza ambaye pia ni Mkurugenzi wa Jiji, Kiomoni Kibamba alikiri kukamatwa kwa vijana wa Chadema Kata ya Lwanima wakidaiwa kuvamia kituo na kuondoka na karatasi za kupigia kura na kwenda nazo mahali pasipo julikana.

**Imeandaliwa na Vitus Audax (MWANZA), Neema Emannuel (MAGU), Remmy Moka (MWANZA), Elizabeth Faustine (MAGU), Restuta Damian (KAGERA), Shaban Njia (KAHAMA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Na Ada Ouko (MUSOMA).**

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe maeneo yaliyoibuka kero katika uchaguzi Serikali za Mitaa

**WANANCHI** katika maeneo mbalimbali nchini, walijitokeza kupiga kura kuchagua viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji. Upigaji kura huo ulifanyika baada ya kukamilika kwa mchakato wa kujiandikisha na kufanya kampeni kwa vyama vilivyosimamisha wagombea katika nafasi za wenyeviti, wajumbe wa kamati mchanganyiko na makundi ya wanawake, wenyeviti wa vijiji na vitongoji kwa maeneo ya vijijini.

Kama ilivyofanyika hamasa kubwa kwa wananchi hao wakati wa kampeni huku Rais Samia Suluhu Hassan akikoleza moto kwa wananchi kujitokeza kutumia haki yao ya kidemokrasia, wananchi walifika kwa wiki katika vito vya kupigia kura kwa wakati, katika baadhi ya maeneo mkoani Dar es Salaam, wananchi walifika kabla ya muda uliopangwa kwa vituo kufunguliwa, yaani saa 2:00 asubuhi.

Pamoja na kuwahi kufika vituoni mapema ili kupiga kura na hatimaye kwenda kwenye majukumu yao, baadhi ya wananchi wasishindwa kutekeleza jukumu hilo la kidemokrasia baada ya kukuta majina yao hayamo kwenye karatasi zilizobandikwa.

Pia wengine walihangaika kupata majina yao kwa kuwa hayakubandikwa kwa alfabeti kama ilivyozoeleka kwenye uchaguzi uliopita. Walipohoji kwa nini hali haikuwa kama wakati uliopita baadhi ya wasimamizi kwenye vituo hivyo walijibu kwamba majina yamebandikwa kama ilivyokuwa kwenye tarehe za uandikishaji, hivyo kuwataka wapigakura kwenye milango mbalimbali ya maeneo ya kupigia kura ili kuangalia majina yao.

Licha ya kuambiwa hivyo, baadhi ya wananchi waliofika mapema kwenye vituo walihangaika kutafuta majina yao bila mafanikio, hivyo kuamua kuondoka bila kupiga kura. Wananchi hao walishutumu utaratibu mbovu uliowekwa ambao walidai umewakosesha haki yao ya kidemokrasia huku wengine wakisema inawezekana ni njama ya kuwafanya wengine kukosa kupiga kura.

Kadhalika, katika baadhi ya vituo, mtu baada ya kuliona jina lake, aliruhusiwa kupiga kura bila wasimamizi na mawakala wa vyama waliokuwa katika vyumba vya kupigia kura kuhakiki jina na kujiridhisha kama mhusika ndiye. Hatua hiyo ingeweza kusababisha mtu yeyote akafanya udanganyifu na kupewa karatasi ya kura na kupiga hatimaye kuondoka zake.

Aidha, katika baadhi ya maeneo, zilitolewa taarifa mbalimbali kuwa baadhi ya wagombea majina yao hayakuwamo kwenye makaratasi ya kupigia kura licha ya kwamba walipishwa kuwania nafasi husika.


Kasoro hizo zilizoainishwa ni ndogo na zinasababishwa na wasimamizi lakini serikali na chama tawala ndivyo vinatwishwa mzigo wa lawama hali inayotia doa mchakato mzima wa uchaguzi na kwenda kinyume cha maagizo ya Rais Samia kuwa kila mtendaji kwenye mchakato huo atende haki.

Kwa ujumla, yako baadhi ya makosa ambayo yanaonekana dhahiri kuwa ni uzembe wa wasimamizi, hivyo mamlaka zilizopewa dhamana ya kusimamia kazi hiyo kuchukua hatua ili kuepusha malalamiko yanayoweza kuufanya mchakato kutokuwa huru na haki.

Ni vyema serikali kupitia Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) hasa wasimamizi wa uchaguzi ngazi za halmashauri, kuchukua hatua dhidi ya wale wote watakaobainika kwa njia yoyote wamesababisha doa katika uchaguzi huo ambao ndilo chimbuko la demokrasia na utawala bora.

Haiwezekani serikali ikatumia mabilioni ya shilingi kuandaa uchaguzi huo lakini watu wachache wautie doa kwa maslahi ya mtu au kikundi cha watu wachache. Watu wa namna hiyo wachukuliwe hatua kwa kuwa kuharibu uchaguzi au kuutia doa lolote ni sawa na uhujumu uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanafunzi 161,020 kukwama kusajiliwa Mtihani Kidato cha Nne, sababu zitolewe

**MNAMO** tarehe 11 mwezi huu, wanafunzi 529,321 wa Kidato cha Nne walianza kufanya Mtihani wa Taifa wa kidato hicho (CSEE). Kwa mujibu wa ratiba inamalizika kesho.

Cha ajabu ni kwamba wanafunzi 161,020 sawa na asilimia 23.3, hawakuwa miongoni mwa watahiniwa hao.

Kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed, aliyoitoa wakati akitangaza kuanza kwa mtihani huo ni kuwa hali hiyo imebinika baada ya kuangalia idadi ya wanafunzi hao walipofanya mtihani wa Taifa wa Kidato cha pili mwaka 2022 walikuwa ambapo 690,341, lakini walioandikishwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne 2024 ni 529,321.

Hii ni dalili mbaya kwenye sekta ya elimu, hivyo kuna haja ya wadau wa sekta hiyo pamoja na serikali kushirikiana kupata taarifa sahihi zizobainisha sababu za wanafunzi hao kushindwa kufanya mtihani huo, ili kuhakikisha jambo hilo halijitokezi tena.

Kiwango cha asilimia 23 ya wanafunzi hao kushindwa kufanya mtihani huo kinazua maswali kwa hakika, licha ya kwamba hata miaka iliyopita kuna idadi ya wanafunzi kadhaa walikwama kufanya mtihani hiyo kitaifa, kwa sababu mbalimbali zikiwamo zilizo nje ya uwezo wao wanafunzi husika au wazazi na walezi kama vile kuugua .

Katika andiko la Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023, inaeleza tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 imeonyesha kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau, ilitekeleza afua mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa fursa za elimu na mafunzo kwa usawa.

Pia, inabainisha afua hizo ni pamoja na utoaji wa elimu bila ada kwa shule za awali, msingi na sekondari kupitia Waraka wa Elimu Namba Tatu ya mwaka 2016; Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi 2021/22-2025/26; Mwongozo wa Kuwarejesha Shuleni Wanafunzi Waliokatiza Masomo Katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa sababu Mbalimbali wa mwaka 2022.

Kwa upande wa elimu ya sekondari, uandikishaji sekondari ya chini (kidato cha I-IV) ulitajwa kuongezeka kutoka 1,675,593 (wavulana 824767; wasichana 850,826) mwaka 2016 hadi 2,645,115 (wavulana 1,248,118; wasichana 1,396,997) mwaka 2022 na kidato cha 5-6 kutoka 131,362 (wavulana 81,129; wasichana 50,233) mwaka 2016 hadi 178,473 (wavulana 99,101; wasichana 79,372) mwaka 2022.

Imebainishwa katia sera hiyo kuwa, ili kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, serikali imeweza kuwarejesha wanafunzi 8,652 masomoni, wanafunzi 6,685 (wasichana) walirejea kupitia utaratibu wa elimu nje ya mfumo rasmi na wanafunzi 1,967 (wavulana 861; wasichana 1,046) walirejea katika mfumo rasmi wa elimu kwa mwaka 2022/23.

Andiko hilo linabainisha kuwa elimu ya sekondari inakusudia kufikia malengo kadhaa ikiwamo kupanua, kuimarisha, na kuendeleza maarifa, stadi, na mtazamo chanya uliopatikana katika ngazi ya elimu ya msingi.

Pia, kuna kumwezesha mwanafunzi kuelewa na kulinda misingi ya utamaduni (mila na desturi), umoja wa kitaifa, tunu za Taifa; na kuthamini haki za binadamu na wajibu unaoendana na haki hizo.

Aidha, kun a suala la kKujenga uelewa wa mwanafunzi kuhusu demokrasia, umuhimu na mipaka yake; kujenga utamaduni na umahiri kwa mwanafunzi katika kujisomea, kujiamini, kujiendeleza kwenye nyanja za sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, kiufundi, kiujasiriamali na kupenda kufanya kazi.

Aidha, kunatajwa; kumwezesha mwanafunzi kutumia stadi za lugha mbalimbali; kumwezesha mwanafunzi kutambua uwajibikaji wa pamoja wa kutunza afya, kuthamini usawa wa kijinsi na kusimamia utunzaji endelevu wa mazingira; kuimarisha misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria.

Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha mhitimu kujiunga na elimu ya juu na mafunzo ya amali sanifu baada ya elimu ya sekondari, kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia mazingira yake.

Kutokana na maelengo yaliyoanishwa hapo, ndipo ninapoona haja ya kutambua mkwamo wa wanafunzi hao, kwa kuwa ni wazi idadi yao watakosa malengo hayo yaliyoainishwa hapo kwa kushindwa kumaliza elimu ya sekondari.

Malengo hayo ni mambo umuhimu, kuanzia binafsi,kwa jamii na taifa kwa ujumla. Naamini sababu zikijulikana, pia wataalam husika watashirikishwa ili kupata ufumbuzi wa kueleweka, ambao utasaidia kuzuia kutokea tena kwa mkwamo huo.

TOLEO MAALUM

# Kwa nini ujiunge na familia ya SimBanking, miamala kidijitali

*CRDB Bank PLC*




*Joseph Alfred Mtata (katikati) kutoka jijini Mwanza naye aliwakilisha maelfu ya Watanzania wanaokamilisha miamala yao kupitia SimBanking baada ya kutangazwa mshindi katika robo ya tatu mwaka huu. Joseph alikabidhiwa zawadi yake na Mkuu wa Idara ya Uendeshaji wa Matawi, Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (wa pili kushoto) pamoja na Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Ziwa, Lusingi Sitta (kulia) wa kwanza kushoto ni Meneja wa Benki ya CRDB tawi la Rock City, Jesca Kikoito. Joseph alikabidhiwa zawadi hiyo katika tawi ya Benki ya CRDB Rock City jijini Mwanza.*

Katika watu wazima zaidi ya asilimia 65 wanaotumia huduma za benki nchini, ni wateja wa Benki ya CRDB pekee wanaofurahia urahisi wa Programu ya SimBanking ndio wanatambulika duniani. Ndio, huu ni ukweli unaothibitika.

Programu ya SimBanking ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za Benki ya CRDB kwenye simu za mkononi, imetambuliwa kuwa programu salama zaidi ya benki kwenye tuzo zilizotolewa hivi karibuni na Jarida la Global Finance lenye makao makuu yake nchini Uingereza.

Benki ya CRDB ilikuwa kati ya taasisi tatu za fedha kutoka Afrika zilizotambuliwa na kutunukiwa katika tuzo za mwaka huu zilizotolewa na jarida hilo maarufu duniani. Taasisi nyingine zilikuwa Benki ya Dashen ya nchini Ethiopia na First National Bank ya Afrika Kusini.

Mwanzilishi Mwenza na Mkurugenzi wa Uhariri wa Jarida la Global Finance, Joseph Giarraputo anasema washindi wa kipengele cha programu bora ya benki walipatikana kwa kuzingatia aina ya huduma wanazozitoa kidijitali, mafanikio waliyoyapata kwa kuwahamishia wateja wao kwenye huduma za kidijitali, uandikishaji wa wateja wapya sambamba na kuwabakiza wale wa mwanzo, na namna majukwaa ya kidijitali yalivyotumika kuboresha biashara, kupunguza gharama na kuongeza tija.

"Kila mshiriki alijadiliwa na jopo la wataalamu wa huduma za benki na mifumo ya Tehama kutoka Infosys, lakini uamuzi wa mwisho ulifanywa na jopo la majaji wetu wa Global Finance. Kutoka Tanzania, Benki ya CRDB imeshinda kwa kuwa benki ya kidijitali," amesema Giarraputo.

Benki nyingi barani Afrika, Giarraputo anasema zimekuwa zikipitia wakati mgumu kutokana na changamoto za kiuchumi kwenye mataifa yao hata hivyo, mikakati iliyowekwa na baadhi ya taasisi hizi za fedha imezisaidia kukabiliana nazo na kuzifanya zivuke salama.

"Badala ya kuanguka na kufilisika kutokana na ugumu uliopo, bado benki hizi zinaendelea udumu na baadhi zinapata faida kubwa hivyo kustahili pongezi," anasema mkurugenzi huyo wa uhariri wa Jarida la Global Finance.

## Mchango wa SimBanking

Mpaka Jarida la Global Finance linatoa tuzo hiyo kwa Benki ya CRDB, taarifa zinaonyesha mafanikio makubwa ya Programu ya SimBanking kwani imechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha matumizi ya huduma za kidijitali ndani ya taasisi hii kubwa zaidi ya fedha nchini ikihudumia pia Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Boma Raballa, Afisa Biashara Mkuu wa Benki ya CRDB ambayo mpaka Septemba 2024 thamani ya mali zake ilikuwa shilingi trilioni 16, anasema benki imeshinda tuzo mbili mwaka huu. Ya pili ni benki bora ya kidijitali.

Kupitia SimBanking ambayo imefanyiwa maboresho kadhaa tangu ilipozinduliwa mwaka 2009, Raballa anasema wateja wa Benki ya CRDB wanapata huduma karibu zote wakati wote na wakiwa mahali popote jambo lililosaidia kuongeza ujumuishi wa wananchi katika huduma za kidijitali.

"Tumepandisha ukomo wa fedha ambazo mteja anaweza kukamilisha miamala yake kupitia SimBanking. Mwanzoni ilikuwa shilingi milioni tano lakini sasa hivi ni shilingi milioni 10. Kiasi hiki kipya kinawawezesha wateja wengi kukamilisha mambo yao kwa wakati. Mteja pia anaweza kuomba mkopo kupitia simu yake na kupata huduma nyingine nyingi," anasema Raballa. Kutokana na urahisi wa kutumia, Programu ya SimBanking imekuwa na manufaa kwa wateja wa nchini hata wanaoishi nje ya Tanzania jambo lililoongeza tija na ufanisi kama inavyothibitishwa na taarifa za fedha za robo ya tatu mwaka 2024 wa Benki ya CRDB.

Taarifa hizo zinaonyesha mikopo iliyotolewa imeongezeka kutoka shilingi trilioni 8.1 Septemba 2023 mpaka shilingi trilioni 10.1 Septemba 2024. Ongezeko hili la mikopo limetokana na kuimarika kwa amana za wateja zilizopanda kutoka shilingi trilioni 8.7 mpaka shilingi trilioni 10.3 ndani ya kipindi hicho.

Mpaka Septemba 2024, Benki ya CRDB ilipata faida ya shilingi bilioni 583.9 kabla ya kodi ikilinganishwa na shilingi bilioni 411.4 zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka jana. Baada ya kulipa kodi, faida hiyo imebaki shilingi bilioni 408.9 ikipanda kutoka shilingi bilioni 280.5 ya mwaka jana. Faida hii ilitokana na matumizi sahihi ya mali za Benki zenye thamani ya shilingi trilioni 16 ambazo zimepanda pia kutoka shilingi trilioni 12.8 zilizokuwapo Septemba 2023.

Matumizi ya majukwaa ya kidijitali yakiongozwa na SimBanking ndani ya Benki ya CRDB yamekuwa na mchango mkubwa katika utoaji na usimamizi wa mikopo. Kwa sasa, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Awali wa Benki ya CRDB, Bonaventura Paul anasema mteja anaweza kuomba mkopo kupitia programu hiyo na akaupata kwenye simu yake wakati huohuo.

Wanaoweza kupata mkopo kwa utaratibu huo, Bonaventura anasema ni wafanyakazi, wanafunzi wa vyuo vikuu wanaopokea mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) pamoja na wastaafu na marejesho yao yanakatwa kwenye akaunti zao tarehe itakapofika.

Kwa watumiaji wote wa SimBanking, anasema upo mkopo wa Jinasue unaoleng akumwezesha mteja kununua umeme, kulipa bili ya maji au kulipia king'amuzi chake na pale inapobidi anaweza akapata fedha taslimu kati ya shilingi 1,000 mpaka shilingi milioni moja.

Kutokana na usimamizi mzuri unaochangiwa, pamoja na mambo mengine, matumizi ya Programu ya SimBanking, ukwasi wa Benki ya CRDB umeongezeka kutoka shilingi trilioni 1.58 zilizokuwapo Septemba 2023 mpaka shilingi trilioni 2.722 mwaka huu. Katika kipindi hicho, benki ilipata shilingi bilioni 321.16 kutokana na ada na kamisheni. Kiasi hiki kinachochangiwa na mapato yatokanayo na huduma za SimBanking kilipanda kutoka shilingi bilioni 257.76 zilizopatikana mwaka jana.

## Wananchi kuzawadiwa na SimBanking

Wakati SimBanking pamoja na majukwaa mengine yakizifanya huduma za Benki ya CRDB kupatikana kidijitali kwa zaidi ya asilimia 96, benki ilizindua na inaiendeleza kampeni inayolenga kuwazawadia wateja wanaofanya miamala mingi kupitia jukwaa hilo.

Bonaventure anasema mteja anaweza kulipa bili mfano ya maji au umeme, kufanya malipo serikalini, kulipia bidhaa dukani, vituo vya mafuta au vinywaji baa, kuuliza salio na mengine mengi bila kulazimika kwenda tawini hivyo kuepuka usumbufu wowote ambao angeweza kukutana nao.

"Mteja anaweza kufungua akaunti kupitia SimBanking. Lengo letu ni kuhakikisha mteja anapata kila anachokitaka mahali alipo na aende tawini kwa mahitaji ya vitu vichache sana vinavyohitaji maelezo ya ziada," anasema Bonaventura na kuongeza: "Huduma nyingi kwa sasa zinafanyika kidijitali duniani hivyo miamala nayo inahamia huko pia. Ni lazima nasi tuungane na dunia, tusiachwe nyuma. Nimwombe kila Mtanzania kuhakikisha anajiunga na Benki ya CRDB ili kutumia huduma hizi salama na zenye uhakika."

Kupitia kampeni ya Benki ni SimBanking yenye kaulimbiu ya 'swahiba, miamala inalipa,' inayolenga kusajili wateja wapya pamoja na kukamilisha usajili wa wateja waliopo ambao hawatumii huduma hii, Bonaventura anasema wateja hushinda zawadi za aina tofauti kutokana na miamala wanayoifanya kila siku.

Zawadi hizo, anasema zinajumuisha gari aina ya Nissan Dualis ambayo ndio kubwa zaidi, linalotolewa kila baada ya miezi miwili, bajaji moja na pikipiki mbili zinazotolewa kila mwezi, simu 10 za kisasa kila mwezi, kompyuta mpakato 10 kila mwezi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini, na fedha taslimu kiasi cha shilingi 30,000 zinazotolewa kwa washindi 32 kila mwezi.

"Wateja wanaotumia huduma za SimBanking wana nafasi kubwa zaidi ya kuibuka washindi. Nawasihi waendelee kufanya miamala mingi kupitia SimBanking ili kujishindia moja kati ya zawadi hizi hivyo kunufaika zaidi," anasihi Bonaventura.

Licha ya zawadi za aina tofauti zinazotolewa, wateja wa SimBanking sasa wanaweza kupata huduma bure wakipiga USSD kwa kubofya *150*03# ili kufurahia huduma wazitakazo tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo ilihitaji kuwa na muda wa maongezi ili kufanya miamala uitakayo.

Ili kutoa nafasi kwa wateja wengi zaidi kujishindia zawadi hizi, Benki ya CRDB imeanza ziara ya kuhamasisha matumizi ya SimBanking kwa Watanzania wote tangu Novemba 15 ikipita katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro.

182718



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali (katikati) akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, Dar es Salaam jana.

# CAG mstaafu, CAG Zanzibar waingia mkataba kuhuisha staili za ukaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar imeingia mkataba wa makubaliano (MoU) na Taasisi ya WAJIBU inayoongozwa na CAG mstaafu Ludovick Utouh, ukilenga kuboresha utendaji ili kuchochea uwajikibaji.

Wawili hao walitia saini mkataba huo wakati wa hafla iliyofanyika jana kwenye ofisi za Taasisi ya WAJIBU zilizoko Mikocheni, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam.

Kabla ya kutia saini mkataba huo, CAG wa Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali aliwaambia waandishi wa habari kuwa Ofisi ya CAG Zanzibar imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na Utouh tangu akiwa CAG, wakianzia kwenye masuala ya michezo na baadaye uhusiano wao ukamea hadi katika utendaji wa kazi za ukaguzi, wakibadilishana uzoefu katika maeneo ya kitaaluma.

"Baadaye tukawa na ushirikiano katika kukagua ile miradi ya maendeleo inayotekelezwa Zanzibar kupitia fungu linalotengwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano, tukawa tunakagua ile miradi kwa pamoja.

"Baadaye tukavuka mipaka ya nchi, tukawa tunakagua balozi kwa pamoja, tulikwenda kwa utaratibu huo kwa miaka mingi. Hata alipostaafu, tuliendelea na utaratibu huo. Tumeendeleza utamaduni huo.

"Baada ya kuwa ameanzisha Taasisi ya WAJIBU, tukaona ni vyema tushirikiane naye akiwa katika taasisi hii, maana anachokifanya ni yaleyale. Tunachokifanya sasa ni kuboresha utendaji ili wananchi wafahamu kinachofanywa na CAG wa Zanzibar.

"Tunapozitoa zile ripoti zetu, walio na elimu kubwa sana, wanakuwa ni wepesi kufahamu zile ripoti. Lakini wale ambao wana elimu za kati na ya chini, inakuwa tatizo. Sasa wote hawa tunataka waelewe ripoti zetu na Serikali ya Zanzibar inafanya nini na inakijita katika jambo gani, ina malengo gani," alisema.

CAG Dk. Abbas kuwa kupitia mkataba huo na Taasisi ya WAJIBU, wanakwenda kufanya ripoti za CAG kuwa rahisi kwa umma; taasisi hiyo itakuwa inatengeneza ripoti ya wananchi kwa njia ambayo itakuwa rahisi kwao kuelewa, ijumuisha matumizi ya katuni.

Alisema kuwa kupitia mkataba huo, watakuwa na fursa za kujengeana uwezo, ikiwamo kubadilishana watendaji ili wafanye kazi kwa pamoja kwa kuwa sheria inawapa rukhsa hiyo. Pia kupeana alichokiita "chaneli za miradi" kwa kuwa Taasisi ya WAJIBU ina uzoefu mkubwa katika eneo hilo.

"Kuna aina za ukaguzi ambazo sisi Ofisi ya CAG Zanzibar tumezianzisha. Aina hizi zinahitaji wataalamu. Kwa mfano, sasa hivi tumeanzisha Forensic Audit (ukaguzi wa kiuchunguzi) hasa kwa makosa ya utakatishaji fedha.

"Kupitia ushirikiano huu, tutapata wataalamu wa kutujengea uwezo. Kama tungehitaji wataalamu kutoka nje, tungelipa fedha nyingi, lakini wenzetu hawa (WAJIBU) watatusaidia," alisema.

CAG Dk. Abbas alisema Zanzibar hivi sasa ina miradi mingi ya maendeleo inayohitaji kuwa na wataalamu kuikagua, akitaja inajumuisha barabara za lami ambazo awali hazikuwapo, shule nyingi za ghorofa, hospitali na ujenzi wa bandari.

"Pia kuna mradi mkubwa zaidi unakuja wa sea taxi (taksi za baharini), unachukua abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hii ni miradi mikubwa ambayo sasa inakwenda kutekelezwa.

"Serikali imekuja na dhana ya uchimbaji mafuta Zanzibar, tayari imeshagundulika mafuta yapo, lazima tuwe na wakaguzi ambao watakuwa na uwezo wa kwenda kukagua mfumo mzima wa uchimbaji mafuta.

"Lakini pia serikali ya awamu ya nane imekuja na uchumi wa buluu. Ni dhana pana sana inayogusa katika maeneo yote. Ni dhana mtambuka kwa sababu kila mtu anaguswa nayo.

"Je, kama Ofisi ya CAG, tumejipanga vipi kuishauri serikali juu ya kutumia malighali iliyomo baharini ili kunufaika nayo na kuongeza pato la nchi na wananchi wanufaike na malighafi hiyo?

"Pato la serikali limekua. Je, wananchi wana hali gani? Tunapaswa kuishauri serikali kuona namna bora ya kuzitumia malighafi kwa lengo la kukuza mapato. Yote haya hayatafanikiwa ikiwa Ofisi ya CAG tutajifungia ndani.

"Hatutofanikiwa kwa sababu hatuna hao wataalamu. Ili tufanikiwe, tumeona tujetuonane na hawa wazee (Utouh na taasi yake ya WAJIBU) ili kupata taaluma yao, fikra zao, mawazo yao. Hivyo, tumeona tuwe na MoU ambayo itatuongoza katika huo ushirikiano," alisema.

**CAG MSTAAFU UTOUH**

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Utouh, alisema matarajio yao ni kuendeleza kazi ambazo wamekuwa wanafanya Tanzania Bara kwa zaidi ya miaka minane kuwaelimisha wananchi ili wawe na uelewa mpana zaidi juu ya dhana ya fedha na rasilimali za umma.

Alisisitiza kuwa bila wananchi kuelewa dhana hiyo, itakuwa shida, hata ulinzi wa mali ya umma utakuwa mgumu, akitolewa mfano; "mtu anakuta watu wanaharibu miundombinu ya shule, anasema 'hainihusu' wakati ile ni mali ya umma na yeye ni sehemu ya umma, hivyo mali ile ni yake".

Utouh alisema, "baada ya makubaliano haya, tutakaa na Ofisi ya CAG Zanzibar na ninaona jambo la kwanza la kufanyika mapema ni kuja na hizi taarifa za CAG ambazo zinaandikwa kwa lugha rahisi, ikichukulia yale mambo muhimu zaidi anayoyajua CAG na kuhimiza serikali na watendaji wake waone umuhimu wa kutekeleza mapendekezo yanayotolewa na CAG.

"Kikatiba na sheria, Ofisi ya CAG ina mamlaka makubwa ya kushauri serikali namna ya kuwa na matumizi bora zaidi ya fedha za umma ili zilete maendeleo kwa wananchi. Fedha za umma zikisimamiwa vizuri, zinanufaisha mwananchi mmoja mmoja na kupunguza umasikini kwa wananchi."

Utouh aliyekuwa CAG kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006, alisema Taasisi ya WAJIBU kwa kushirikiana na Policy Forum wamepata ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) ambao utekelezaji wake unagusa Tanzania Zanzibar na Tazania Bara, hivyo mkataba waliotia saini jana unarahisisha kutekeleza majukumu yao Zanzibar.

**POLICY FORUM**

Mkurugenzi Mtendaji wa Policy Forum, Semkae Kilonzo, alipongeza Taasisi ya WAJIBU na CAG Zanzibar kwa kufikia makubaliano hayo ambayo anaamini yataboresha utendaji wao na kuongeza uwabikaji serikalini na kuchochea ushiriki wa wananchi katika kudai haki na uwajibikaji wa watendaji.

"Nimefurahishwa na maelezo ya CAG Dk. Abbas namna wanavyojipanga kushirikisha wananchi katika mchakato mzima wa ukaguzi wa fedha za umma katika taasisi.

"Kuziweka hizi taarifa kwenye lugha nyepesi ni jambo jema sana. Kuandaa ripoti nzuri ni jambo moja, lakini wananchi kuzielewa na kuzitumia ripoti kudai haki na uwajibikaji ni jambo muhimu," alisema Kalonzo.

Taasisi ya WAJIBU mbali na kuchambua ripoti za CAG na kutoa ripoti za uwabikaji zinazokuwa na lugha rahisi, pia imekuwa inaandaa semina na warsha kwa wabunge, waandishi wa habari, maofisa wa wizara na taasisi za serikali, wanafunzi na wananchi wa kawaida kuwajengea uwezo kutambua wajibu wao kwa lengo la kuchochea uwajibikaji wa mamlaka za serikali na ushiriki wa wananchi katika kudai uwajibikaji huo.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



## Bilioni 40/- kutanua wigo wa mawasiliano vijijini

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

ZAIDI ya Dola za Marekani milioni 15 (Sh. bilioni 39.8) zimepangwa kutumika kuwekeza katika utanuzi wa wigo wa mawasiliano ya mtandao, kwa kaya milioni 14 zilizoko vijijini.

Hadi kufikia sasa kaya 300,000 pekee ndizo ndizo zilizounganishwa na mtandao wa bei nafuu kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA), pembezoni mwa mikoa ya Tanzania.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Mawingu, Farouk Ramji, akizungumza na wadau mbalimbali jana jijini Arusha, alisema wamepanga kuwafikia watu milioni moja ifikapo mwaka 2028 waishio vijijini.

"Tutatumia Dola za Marekani milioni 15, kuleta mtandao wa bei nafuu kwa kaya za vijijini nchini Tanzania, ambapo ni kaya 300,000 pekee kati ya milioni 14 ndizo zilizounganishwa," alisema.

Uamuzi wa kampuni hiyo unatokana na kuinunua kampuni ya habari inayotoa huduma ya Teknolojia ya Habari na Mawasilaino (TEHEMA), pembezoni mwa mikoa ya Tanzania kwa zaidi ya miaka 25.

"Leo ni siku muhimu sana kwa soko la mawasiliano Afrika. Kwa kushirikiana na habari, hatupanui tu wigo wetu, bali pia tunathibitisha dhamira yetu ya kuunganisha jamii za vijijini na zile za pembezoni.

...Tunalenga kutumia mafanikio yake yaliyoyapata nchini Kenya kwa kushirikiana na wataalamu wa ndani wa habari, huku lengo likiwa ni kupanua shughuli na athari zake kote Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla, hatimaye kuunganisha watu milioni moja ifikapo mwaka 2028.

Aliongeza kuwa ununuzi huo unaonyesha pengo la kidijitali linaloendelea kuwapo Afrika Mashariki ambako wateja wa vijijini hawahudumiwi ipasavyo au huduma za mtandao ni ghali mno.

Ofisa Mkuu wa Uwekezaji wa Infra Co Africa, Claire Jarratt, alisisitiza umuhimu wa sekta binafsi katika kufanikisha muunganisho wa kidijitali.

# Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni kuongezewa hadhi

**Na Godfrey Mushi,**
MONDULI

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imeanza mchakato wa kuiongezea 'hadhi' Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni iliyoko mkoani Arusha.

Lengo ni kuwavutia watalii wengi zaidi hasa wakati wa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) la mwaka 2027.

Makuyuni Wildlife Park, ambayo imeanzishwa mwaka huu, itakuwa na bustani ya wanyamapori ya kipekee katika nchi za Afrika, utalii wa night game drive, utalii wa ndege wa kipekee walioko eneo hilo, utalii wa kupanda balloon, utalii wa kutembea kwa kupanda milima, bush dinner, walking safaris na utalii wa kitamaduni.

Jana, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAWA, Dk. Simon Mduma, alisema hifadhi hiyo mpya itaongeza mapato kwa muda mfupi katika mashindano ya AFCON, ambapo Arusha itapokea wageni wengi kutoka mataifa mbalimbali.

"Tumeanza rasmi utekelezaji wa mikakati ya kuiendeleza na kuiandaa Hifadhi ya Makuyuni Wildlife Park, kwa ajili ya kupokea wageni wengi zaidi, kwa kuongeza mindombinu ya utalii hususani barabara, ujenzi wa mabwawa ya maji na kuondoa mimea vamizi ndani ya eneo hilo.

"Mimi na bodi yangu, tumezunguka na tumeona maendeleo ya ujenzi wa barabara, ni kazi ambayo inaridhisha; ni nzuri na ratiba ambayo ipo kwa makubaliano kwenye mikataba kazi ya ujenzi wa barabara inaendelea vizuri sana," alisema.

Hifadhi hiyo imeanzishwa, baada ya Oktoba mwaka 2023, serikali kuyatwaa mashamba matatu makubwa, maarufu kama mashamba ya 'STAIN' yaliyokuwa yakimilikiwa na mwekezaji raia wa kigeni katika Wilaya ya Monduli.

Mashamba hayo ni Amani lenye ekari 9,007, Lente ekari 3,344 na Loldebes ekari 2,812, ambayo kwa sasa yanatumika kama eneo maalum la kuendeleza shughuli za uhifadhi na utalii.

Inaelezwa kwamba, uamuzi wa serikali ulichagizwa na hali ya utulivu wa mashamba hayo yaliyopo kwenye ushoroba unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Manyara, Ranchi, Ziwa Manyara na Msitu wa Hifadhi wa Essimingor, ambao hupenda kutumiwa na wanyama kama eneo la mazalia.

Alisema: "Hifadhi hii ni mpya, ilikabidhiwa takribani mwaka mmoja uliopita, ilikuwa na uhitaji wa kuongeza barabara ili wageni watakaokuwa wanatembelea eneo hili, wawe na wigo mpana wa kuiona mandhari nzuri; na vilevile kutoa nafasi kubwa ya kuona vivutio ambavyo vipo kwenye hifadhi hii," alisema Dk. Mduma.

Aidha, Dk. Mduma, alisema eneo la Makuyuni kabla ya kutwaliwa, lilikuwa likikumbwa na changamoto ya ukame wakati wa kiangazi, kiasi cha kusababisha wanyamapori kutoka nje ya hifadhi hiyo na kwenda kwenye makazi ya watu.

"Bodi ya TAWA, iliona umuhimu wa kujenga bwawa la kukusanyia maji kwa ajili ya wanyamapori, hivyo bodi hiyo imefanya ukaguzi wa eneo litakapochimbwa bwawa hilo na kuridhishwa nalo na hivyo ujenzi wake utaanza hivi karibuni kwa kuwa mikataba imekwisha sainiwa tayari kwa kuanza kazi hiyo," alisisitiza.

Mjumbe wa bodi hiyo, Prof. Suzanne Augustino, aliipongeza menejimenti ya TAWA kwa jitihada kubwa wanayoifanya kuboresha mazingira ya Makuyuni Wildlife Park, ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi ushauri na maelekezo yanayotolewa na bodi inayoongozwa na Mwenyekiti Meja Jenerali (mstaafu), Hamis Semfuko.

Naye Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, ambaye pia ni Kaimu Kamanda wa Uhifadhi Kanda ya Kaskazini ya TAWA, Privatus Kasisi, alisema kitendo cha serikali kuiamini na kuikabidhi eneo hilo muhimu kumeipa chachu na nguvu ya kuliendeleza na kulisimamia kwa ukamilifu ili kulifanya liwe bora kwa manufaa ya wakazi wa Mkoa wa Arusha na taifa kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Kamanda wa eneo la Makuyuni Wildlife Park, Andrew Kishe, aliieleza bodi hiyo kuwa miradi yote inayotekelezwa na TAWA ndani ya hifadhi hiyo inagharimu zaidi Sh. bilioni moja.



Dereva wa mtambo wa kuchimbia akisawazisha vifusi katika Kanisa la Wamisionari wa Mapadre wa Passionist Fathers kijijini Zeneth, wilayani Muheza. Eneo hilo limepitiwa na mradi wa bomba la mafuta ghafi la EACOP, hivyo baadhi ya majengo yao yamebomolewa ili kupisha utekelezaji wa mradi huo. **PICHA: CHEJI BAKARI**

# Matukio ya ukatili 7,893 yaripotiwa Manyara

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MKOA wa Manyara unatishiwa na kasi ya ongezeko la ukatili dhidi ya wanawake na watoto baada ya kuripotiwa matukio 7,893 katika kipindi kisichozidi miezi 10.

Huku, Ripoti ya Hali ya Afya na Demografia Tanzania (TDHS), ikionyesha chanzo cha ukatili huo, asilimia 60 unatokea ndani ya familia na asilimia 40 unaotokea shuleni.

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili mkoani humo, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Mkoa wa Manyara, Anna Fisoo, alisema ukatili huo umeripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka huu.

Kwa mujibu wa Fisoo, ukatili unaofanyika katika jamii, unasababisha serikali kutumia zaidi ya Dola za Marekani milioni sita, ili kutibu waathirika wa ukatili kupitia mpango mkakati wa taifa wa kutokomeza ukatili.

Alisema: "Ulawiti siku hizi umekuwa fasheni katika jamii, lakini hiyo yote inasababishwa na wazazi kukosa umakini kwa watoto wao wengi wao wako busy na vikoba na kutafuta hela".

Aidha, Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi, Wilaya ya Babati, Daudi Danyesi, alisema mafanikio ambayo wameyapata toka kitengo hicho kianzishwe ni kuongezeka kwa uelewa katika jamii, wanaofanya ukatili kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa na mwitikio wa kuripoti matukio ya ukatili kuongezeka.

Awali, Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema ni vizuri sheria na sera ziimarishwe ili kusaidia kupinga ukatili wa kijinsia.

Konki alisema ni wakati wa kuhakikisha waathirika wa ukatili wanapata haki zao na ni lazima kubaini mila potofu ambazo zinaendeleza ukatili.

Askofu huyo alisema waandishi wa habari wanayo nafasi kubwa ya kupaza sauti kwa kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Kenneth Simbaya, aliiomba serikali inapopanga mipango ya maendeleo kuanzia hatua za awali iwashirikishe waandishi wa habari ili waweze kusaidia jamii.

Alisema asilimia 58 ya wanawake na asilimia 40 ya wanaume waliohojiwa kuhusu wanawake kupigwa walisema wapigwe.





# DC aagiza kampeni kupinga ukatili kuanzia nyumbani

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele ameyaagiza mashirika yasiyo ya kiserikali kuhamishia kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia katika ngazi ya familia kutokana na vitendo hivyo kukithiri katika wilaya hiyo.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia katika kituo cha kulea wasichana cha Massanga.

Alisema siku za nyuma mashirika na taasisi za kiraia zinazoendesha programu za kupinga ukatili huo wamekuwa wanafanya shughuli zao maeneo ya mjini na kushindwa kuwafikia walengwa halisi wanaopatikana vijijini.

"Tunatakiwa kujikita zaidi maeneo ya pembezoni ambapo waathirika wengi wa matendo hayo wanapatikana na taarifa zao hazifiki katika vyombo husika kutokana na kufanywa kuanzia ngazi ya familia," alisema Gowele.

Akitoa mfano alisema baadhi ya wazazi walioshirikiana na ngariba na wazee wa mila kuwafanyia watoto wao wa kike ukeketaji na kisha kusababisha ndoa za utotoni na madhara mengine yakiwamo ya kiafya.

Aliagiza pia tohara inayofanywa kwa vijana wa kiume ifanyike kwa njia zilizo salama ili kuwakinga na maradhi na athari nyingine kama vile kupoteza damu nyingi.

Alisema serikali ya wilayani itawachukulia hatua kali ngariba na wazee wa mila ambao watashiriki katika zoezi la ukeketaji ambapo kila baada ya miaka miwili jamii eneo hilo hutekeleza kwa wasichana wadogo.

Meneja miradi wa kituo cha ATFGM Massanga, Valerian Mgani alisema kila baada ya miaka miwili takribani wasichana 200 hukimbilia hapo kupata hifadhi na ushauri.

Alisema wasichana hao wanaelekezwa mbinu za kupambana na ukatili dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuunda vikundi rika kwa ajili ya kutoa taarifa za matendo hayo kwa waalimu, wazazi na katika vituo vya polisi.

Ofisa wa polisi kutoka Dawati la Jinsia Mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya, Jumanne Mkwama, alisema baadhi ya waathirika wa matukio ya ukatili wanaogopa kutoa taarifa na ushahidi kwa kuogopa kutengwa na familia zao wakirejea majumbani kwao.

"Isitoshe baadhi yao pia huogopa kutoa ushahidi mahakamani ili haki ipatikane kwa muda muafaka na hivyo kusababisha matendo ya ukatili wa kijinsia kuendelea kushamiri katika baadhi ya jamii maeneo haya," alisema.

Mganga Mkuu Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Amini Vasomana, alibainisha madhara ya kiafya yatokanayo na ukeketaji kuwa ni pamoja na kutokwa damu nyingi inayoweza kusababisha kifo pamoja na magonjwa ya kuambukizwa kama vile ya zinaa.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa katika mstari na wananchi mbalimbali wakati akishiriki kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa Kitongoji cha Kihanga, Kijiji cha Kasumo, Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Halmashauri ya Sengerema yakabiliwa uhaba madawati

**Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Sengerema, Binuru Shekidele, amesema halmashauri hiyo ina upungufu wa madawati zaidi ya 12,000 katika shule za msingi.

Shekidele alibainisha hayo juzi wakati wakikabidhiwa madawati, meza na viti 1,131 na mgodi wa Sotta Mining wa Nyanzanga na kuwa zipo jumla ya shule za msingi zipatazo 115 za serikali na kwamba madawati yatatolewa katika shule za msingi 37 katika halmashauri hiyo.

Shekidele alisema waliamua malipo yote yatengeneze madawati ambayo yataenda kutumika katika shule tarajali ya Sekondari Rubungo ambayo inatarajiwa kufunguliwa mwakani.

Akikabidhi madawati hiayo, Ofisa Uhusiano wa mgodi huo, Habiba Saidi, alisema wametengeneza hizo zenye uwezo wa kubeba wanafunzi watatu kwa kila dawati, viti vinane na meza 14 kwa ajili ya matumizi ya walimu.

Pia, yatatengeza madawati 160 yenye uwezo wa kukaa mwanafunzi mmoja, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 93.420.

Akipokea madawati hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, alisema waliyotoa ni uhusiano na halmashauri kwani bado mgoni haujaanza kufanya kazi na kusema pale mgondi utakapoanza kufanya kazi lazima ufuate kanuni.

Hivyo, alimtaka Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya hiyo kutafuta kanuni ili wazisome na waende kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi kuunda kamati itakayohusika katika kujadili maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi

Mtanda alisema kampuni zote zilizopo katika Halmashauri ya Sengerema na Buchosa yanatakiwa kuiga mfano huo ili kusaidia idara ya elimu, siyo kwa kutoa madawati hata kwa kutoa mahitaji kwa wanafunzi ambao hawana uwezo.

Alisema pia wanaweza kutoa msaada wa kuwahudumia wanafunzi kwa kuwanunulia sare pamoja na vitu vya msingi na kusaidia jamii hata idara ya afya.

# Adakwa akiuza magunia 30 ya mbegu za pamba

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Shinyanga linamshikilia Juma Mtobela, kwa tuhuma za kuuza mbegu za ruzuku za pamba gunia 30 katika Kijiji cha Maganzo wilayani Kishapu.

Mtobela anadaiwa kuuza mbegu hizo kwa mtu ambaye hakufahamika na alitokomea kusikojulikana, huku akiendelea kusakwa na Jeshi la Polisi.

Hayo yalibainishwa juzi na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari na kusema mtuhumiwa huyo alikamatwa Novemba 23, mwaka huu.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi limewakamata wahamiaji haramu saba ambao ni raia wa Burundi, katika Kijiji cha Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu katika Wilaya ya Kahama, kwa kosa la kuingia nchini kinyume cha sheria na wamewapeleka katika ofisi za uhamiaji kwa hatua zaidi za kisheria.

Alisema Jeshi la Polisi limewakamata watu 51 kwa tuhuma za wizi pamoja na vielelezo mbalimbali zikiwamo bangi kilo 10, pikipiki tisa, pombe aina ya moshi lita 15, magodoro manne, kontena mbili za bati, mashine tatu za bonanza, gari likiwa na nondo 130.

Zingine ni binding wire 11, mifuko 100 ya saruji, simu mbili, redio saba, kabati, friji na kitanda kimoja.

Alisema Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, limefanikiwa kukamata madereva mbalimbali, kwamba makosa ya gari ni 5,615, bajaji na pikipiki ni 2,305, huku wakimfikisha mahakamani dereva mmoja kwa kosa la kuendesha gari akiwa amelewa na kuhukumiwa kifungo cha mwaka mmoja.

**Mtobela anadaiwa kuuza mbegu hizo kwa mtu ambaye hakufahamika na alitokomea kusikojulikana, huku akiendelea kusakwa na Jeshi la Polisi.**

ama

ALHAMISI NOVEMBA 28, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**WAKUTANISHWA HOSPITALI MUHIMBILI... Simulizi wimbi la mateso ya uzazi, ndoa kwa wanaolea wenye kifafa**



**Mtaalamu afya na darasa la kina uzazi mpango hadi usalama wake**

Ukurasa 13

## KAZI IKIENDELEA UKINGONI MWA 2024...

# Ilivyo safari yake Samia kitabibu, dhamana tiba mpya kwa wagonjwa

## •Jicho kuu; kufuta kigugumizi cha kumfikia mhitaji

**Na Mwandishi Wetu**

SAFARI ya kuwa na Watanzania wanaopohudumiwa kisheria na bima ya afya imeiva, hata kufikia kwenye utekelezaji wa ndoto ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Imekuwa likishuhudiwa kwa hatua za utekelezaji wa serikali yake, akiwa na wastani wa miaka miwili na nusu madarakani, Wizara ya Afya chini ya utawala wake ikatinga bungeni Novemba 2023 na Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Hapo inakuja baada ya kukwama miezi sita kabla, mnamo mwezi Februari 2023 kwa hoja iliyotolewa na bunge ya kutokuwapo chanzo endelevu cha fedha kutekeleza mpango huo.

Kimsingi, ndani ya ndoto hiyo ya miaka mingi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imekuwa na dhima kuu kiafya kutoa huduma bora kuanzia ngazi msingi hadi taifa, ikitazamia wananchi watapata huduma bora na kwa karibu zaidi waliko.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya, Wadau wa Sekta na wataalamu wengine, tayari wamefanyia kazi hoja zote zilizoibuliwa na bunge, pamoja na wadau.

"Hata hivyo, semina zimefanyika kwa makundi mbalimbali ndani ya jamii kuhusu umuhimu wa Bima ya Afya kwa wote," akatamka, Englibert Kayombo, msemaji wa wizara hiyo.

**KUTOKA WIZARANI**

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Afya, Amoury Amoury, anasema mpango huo wa Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia, una manufaa ya kudhibiti kuongezeka magonjwa yasiyoambukiza, hata kuwawezesha wananchi kumudu gharama za matibabu.

Amoury ametamka wiki mbili zilizopita jijini Dodoma, katika Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza, katika kikao kazi cha kujadili mikakati ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza nchini, ikihusisha wizara 15 za kisekta na wadau mbalimbali.

Amoury anaitaja Bima ya Afya itawasaidia wananchi kudhibiti ongezeko la magonjwa hayo yasiyoambukiza, kila mwananchi akipata huduma za uchunguzi na matibabu, penye mahitaji pasipo kikwazo cha fedha.

"Sheria hii ya bima ya afya kwa wote pia itamkinga mwananchi kulipia huduma ambazo zinaweza kumsababishia umaskini, tumeshuhudia baadhi ya wananchi wasio na bima ya afya wakiuza mali ili waweze kugharamia matibabu," anaeleza.

Mkurugenzi huyo anaongeza: "Wananchi walio na Bima ya Afya hadi sasa ni asilimia 15, asilimia 85 ya wananchi (nchini) hugharamia matibabu kwa malipo ya papo kwa papo."

Anarejea Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kuwa, inamlazimisha kila mwananchi kuwa mwanachama wa bima ya afya nchini, hata anatibiwa bila ya kikwazo, hata pale anapokuwa katika hali mbaya.

"Mwananchi ataenda hospitali mapema kabla ya kuwa na tatizo kubwa la ugonjwa, hivyo kutibiwa mapema na kuokoa gharama kubwa," anaongeza Amoury.

Mnamo Julai mwaka huu akiwa mkoani Katavi, Rais Dk. Samia, akatoa wito kwa wakazi wake na Watanzania kwa ujumla, wajitahidi kuwa na Bima ya Afya, kila mwananchi anunue bima yake na familia zao, hata kuwaepushia usumbufu.

"Niwaombe sana watakapokuja Mfuko wa Bima ya Afya, kila mwananchi anunue bima yake na familia yake. Maana yake unakata bima yako mara moja kwa mwaka unatibiwa mwaka mzima," anatamka, akigusa mafanikio mojawapo ni uhakika wa matibau kwa wanachama hai.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akihutubia tukio linalohusu Bima ya Afya. **PICHA: MTANDAO.**

**YANAYOSIMAMIA BIMA AFYA**

Tarehe Mosi ya mwezi huu, kulihitimishwa Kongamano la Siku Nne la Bima ya Afya kwa Wote na Jukwaa la Ugharamiaji Huduma za Afya, huko limehitimishwa Novemba Mosi 2024, huko mkoani Arusha.

Ilichukua nafasi kwa wataalamu na wadau wa sekta ya afya, kukabiliana kutekeleza maazimio saba ya kusaidia utekelezaji wa huduma za Bima ya Afya kwa Wote, anayoyataja kuwa ni:

* Azimio la kwanza; wataalamu wa sekta kukubaliana kutumia utaalamu wao kupata au kuongeza rasilimali fedha kutoka vyanzo mbalimbali, kugharamia utekelezaji wa bima hiyo.

* Kuandaa mkakati unaobainisha majukumu na wajibu wa wadau wote wa afya, ikisisitizwa si jukumu la sekta ya afya pekee.

* Wataalamu kuhakikisha viwango vya uchangiaji kwa wanachama vinazingatia uwezo na kuwa na namna bora ya uchangiaji, husuan kwa sekta isiyo rasmi.

* Kuandaa mpango mkakati wa ulazima wa watu wote kujiunga na bima hiyo.

*Mpango shirikishi wa utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima ya hiyo, ikiwashirikisha wadau wote.

* Uimarishwaji matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA), kuwawezesha kutekelezawa Bima ya Afya kwa Wote, hususan usajili wa wanachama na vituo, uwasilishaji, uchakataji na ulipaji madai.

* Serikali kuendelea kuwashirikisha wadau katika dhana nzima ya utekelezaji wa bima hiyo.

Hiyo inafanyika huku wadau wa sekta ya afya wakiahidi kuendelea kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na kutoa msaada wa kitaalamu na rasilimali katika uanzisha vyanzo endelevu vya

Inaendelea Uk. 14

AFYA

## WAKUTANISHWA HOSPITALI MUHIMBILI...

# Simulizi wimbi la mateso ya uzazi, ndoa kwa wanaolea wenye kifafa

## •Wazazi kiume na kashfa kukimbia wenza

**Na Christina Mwakangale**

HADI sasa kunalalamikiwa unyanyapaa dhidi ya wanaougua kifafa, hata kugeuka pingamizi kwa wazazi wa watoto wenye ugonjwa, pale kundi hilo linapotaka kupiga hatua.

Kuna simulizi ya kinamama wawili miongoni mwa wanaolea watoto wenye kifafa, wanayoilezea Nipashe mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, kuhusu madhila wanayopitia kuwa wazazi wa watoto hao.

Hiyo ni katika kongamano la kitaifa lililoandaliwa Chama cha Wazazi Wenye Watoto wenye Kifafa Tanzania (UWAKITA), kwa kushirikiana na Idara ya Afya ya Akili Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ikiwakutanisha wazazi hao, wataalamu wa afya na waandishi wa habari.



Mtoto mwenye umri wa miaka nane, aliyepooza baadhi ya viungo, pia ana kifafa akiwa na mama yake wakipaka rangi katika mchoro. **PICHA: UMOJA MATAIFA.**

**SIMULIZI ILIVYO**

Glory Mrema na Avelina Said, wote ni walezi wa upande mmoja yaani kitaalamu 'single mothers', baada ya wenza wao, mmoja kumtelekeza mwenzake na mwingine amefiwa na mzazi mwenza, Agosti mwaka huu.

Glory ni mkazi wa Ubungo, Dar es Salaam, akiwa miongoni mwa kinamama wanaougua ugonjwa huo, baadhi wameacha kwenda hospitali kuhudhuria kliniki na kutopata dawa zaidi ya miezi tisa.

"Nashindwa kumudu gharama hizo tangu bima ya watoto iliposititishwa na serikali. Ombi langu kwa serikali, watoto wanaoishi na hali ya kifafa tuwalipie hata bima ya 'Toto Afya Kadi', ili wahudhurie kliniki. Ombi letu kwa Rais Samia.

"Kidonge kimoja cha miligramu 500 kinauzwa Sh. 1,500 kwa bei ya rejareja. Mtoto mmoja anapaswa kumeza vidonge vinne kila siku, yaani viwili asubuhi na viwili jioni, bado dawa ya usingizi ambayo kidonge kimoja kinauzwa Sh. 500. Kwa siku moja mgonjwa wa kifafa anatumia Sh. 6,500.

"Kilio changu kwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan atuangalie kwa jicho la pekee, watoto wanaoishi na kifafa usalama wao ni dawa na chakula. Kama mtoto mwenye hali hiyo hajanywa dawa, ndani hapakaliki.

"Anafanya fujo nyumbani, tunashindwa kutoka katika shughuli za kutafutia kipato, tulio wengi tumeachwa na waume zetu baada ya kupata watoto hawa, " anasema Glory.

Avelina, mkazi wa Mbezi Louis, Dar es Salaam, pia ni mzazi mwenye mtoto anayeishi na kifafa, sasa ana umri wa miaka 17, aliyeanza kuugua tangu akiwa na miaka sita. Kilio chake, kwa serikali ni kupata matibabu ya uhakika kwa mtoto wake.

Anasema, gharama za dawa kwa siku moja ni takribani Sh. 6,000, hana kipato cha uhakika, akitegemea kuuza karanga anazopeleka dukani kwa mtu, kutokana na kushindwa kutoka nyumbani kuziuza mwenyewe, kwa kuwa hana mtu wa kumuachia mtoto.

"Mume alifariki Agosti, mwaka huu. Karanga nazitengeneza nakaanga, napeleka dukani kwa mangi anaisaidie kuuza, kwa sababu nikitoka nitamwachia nani mtoto, unahitaji kumhudumia kuanzia kwenda choo, umlishe, umuogesha, shuleni aliambiwa asiende tena," anasema Avelina.

Hivi sasa, mwanawe anayemtaja kwa jina la, Immaculata William ana umri miaka 17, anayeishi ndani kwa kutegemea misaada, hata anapoonewa huruma hununuliwa dawa wastani siku tano au nusu mwezi na zinapokwisha, hali ya mtoto inabaki mbaya.

"Alikuwa anasoma shule ya msingi Kibamba (wilayani Ubungo), lakini hawezi kutembea, wakasema labda nimpeleke shule maalum iko Mbagala.

"Nikaona atahudumiwaje na walimu? Kwenda chooni hadi nimbebe. Tulikuwa tunatibiwa kwa bima, ambayo ililipiwa na mzazi mwenzangu, sasa kafariki.

"Kwa siku 15 anatumia vidonge vya sh. 45,000 dozi yake ni asubuhi na jioni. Asipokunywa siku hiyo hakukaliki ndani. Niliambiwa kwenye ubongo wake kuna ufa. Alizaliwa vizuri ila alipofikisha miaka sita mwaka 2007, tatizo lilianza.

"Ombi langu kuu sisi wenye watoto wanaotegemea kuishi kwa dawa, serikali ituangalie kwa jicho la kipekee tupate hiyo bima ya watoto, ili watibiwe kwa uhakika.

"Tangu Machi mwaka huu, sijampeleka mtoto kliniki bima ya NHIF kifurushi cha 'Toto Afya' cha Sh 50,400 kilituokoa wazazi wengi," anaeleza Avelina.

**UNYANYAPAA ULIPO**

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Kuganda Said, anasema bado inahitajika elimu kwa umma, kuhusu ugonjwa wa kifafa na kwamba dawa na wataalam wapo na ugonjwa unatibika.

Anasema kuna takwimu ambazo bado hazijawekwa hesabu zake katika data, ila kati ya wanaohudhuria kliniki ya Afya ya Akili MNH, wako kinamama zaidi huugua magonjwa ya akili kama msongo wa mawazo.

Bingwa huyo anafafanua kutokana na hali hiyo, baadhi wakihojiwa, hueleza baada ya kujifungua watoto wenye tatizo la kudumu kiafya kama kifafa, wenza wao huwatelekeza, akisema husababisha msongo wa mawazo na ongezeko la 'single mothers' kwenye jamii.

Mwenyekiti wa UWAKITA, Dk. Kuganda, anasema chama hicho kinasisitiza elimu ya ugonjwa huo na jamii ielewe kwamba wataalam wa kifafa wapo, vifaa vya uchunguzi navyo vipo, huku kifafa kinatibika, hivyo anawaasa watu waache unyanyapaa, kitendo kinachotawala dhidi ya kundi hilo.



Avelina Saidi, mama mwenye mtoto anayeugua kifafa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

"Kifafa kinakumbwa na unyanyapaa zaidi. Wanaougua msisitizo ni wapewe fursa sawa bila kubaguliwa yaani kupata tiba ya uchunguzi na dawa, ili wasijihisi unyonge," anasema.

**HATUA KUWAKOMBOA**

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili MNH, Nuruel Kitomary, anasema zaidi ya watu milioni 50 duniani wanaishi na kifafa na asilimia 80 wanatoka nchi zenye uchumi mdogo barani Afrika, ikiwamo Tanzania.

"Kati ya hao, watu milioni 10 wanaishi Afrika na Tanzania inakadiriwa kuwa na watu 450,000 mpaka 500,000 wanaoishi na kifafa. Ni asilimia 3.7 pekee ndiyo wapo kwenye matibabu.

"Hawa ni wale wenye usajili rasmi hospitalini, lakini kuna kundi kubwa nje ya hao, ambao wamefichwa majumbani au wapo kwa waganga wa kienyeji, makanisani," anasema Dk. Kitomary.

Anafafanua kwamb, tangu Machi mwaka huu, kumekuwako ukuzaji uelewa kuhusu ugonjwa huo, kupinga unyanyapaa na kuwapo mtazamo kwa watunga sera kulitambua kundi hilo lipewe.

"Magonjwa ya mishipa ya fahamu ikiwamo kifafa yanaongoza kwa kusababisha ulemavu na sababu ya pili ya chanzo cha vifo.

"Mitazamo hasi juu ya wenye kifafa, inawafanya waishi nusu ya maisha yao 'not to the fullest' (yasiyo kamili), kwa sababu ya unyanyapaa kwenye jamii na wao pia hujinyanyapaa.

"Asilimia 86 ya wanaougua hawako huru, wanatengwa asilimia 44 kati yao wanapitia katika unyanyapaa kama vile shuleni, kazini, majumbani na kila mahali.

"Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 nayo inaongeza unyanyapaa kwa sababu kuna kipengele kimeeleza kuachana mwenza mara tu atakapobainika kuwa ana kifafa.

"Wanakumbana na unyanyapaa kijamii, kwa imani potofu; kimfumo kwa kukumbana na vikwazo katika huduma za afya; wanajihisi aibu na wasio na thamani," anasema.

Bingwa huyo anasema, kunahitajika tafsiri ya kisera kutoka kwa watunga sera kuhusu haki ya elimu kwa mtoto, kwa sababu watoto wanaougua wakiwa shuleni wanaambiwa warudi nyumbani na kukosa haki hiyo.

**Inaendelea Uk. 13**

AFYA

# Mtaalamu afya na darasa la kina uzazi mpango hadi usalama wake

**Na Joyce Lameck**

KATIKA jamii sasa kila kona kunanadiwa dhana iliyobebwa na wengi kuhusu matumizi ya njia za uzazi wa mpango zinazobatizwa 'za kisasa' kwa kukiuka kanuni za afya.

Nyingi zinatajwa si sahihi na zinachangia madhara, hata kusabisha vifo vitokanavyo na uzazi usio salama.

Hiyo ni baada ya utafiti uliofanyika na kugundua kitakwimu kwamba, nusu ya mimba zote zinazotungwa duniani hazikutarajiwa.

Hapo ina maana kuwa takriban wanawake milioni 121 kila mwaka hupata mimba zisizopangwa kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) mwaka 2022.

Hivyo inatajwa kuchangia kuwapo takribani asilimia 60 ya mimba hizo huishia kutolewa, huku asilimia 45 ya utoaji mimba huo unakuwa si salama. Hapo inatajwa kuchangia asilimia tano hadi 13 ya vifo vya wajawazito duniani kote.

Kwa upande wa Tanzania, inatajwa kati ya mwaka 2015 na 2019, kulikuwapo jumla ya mimba 2,930,000, takribani nusu yake hazikupangwa.

Vilevile inaelezwa kuwa asilimia 40 ya mimba hizo zimeishia kutolewa katika mazingira ambayo hayakuwa salama.

Mbadala sahihi unatajwa kutumia uzazi wa mpango, unaotajwa kuwa katika nafasi ya kusaidia kupunguza na kutokomeza mimba zisizotarajiwa.

Vivyo hivyo, inatajwa kitalam mafanikio katika utoaji mimba ni pale itafanyika kwa namna sahihi na inayozingatia mbinu na kanuni za utoaji mimba salama, kumnusuru mwanamke husika.

### MTAALAM AFYA

Mtaalam na mtoa huduma za afya ya uzazi,



Mama akimwongoza binti yake anayenyonyesha mtoto. Ni sehemu ya tafsiri pana inayohusu uzazi wa mpango na malezi. **PICHA: MTANDAO.**

Mgeni Kisesa, anasema kuna umuhimu kwa kinamama kutumia njia za uzazi wa mpango, kwani zina faida kwao na hata taifa kwa ujumla.

Pia, anaeleza sababu za mwanamke kushauriwa kutumia njia za uzazi wa mpango, wakati anapofanya mapenzi na mwanaume.

Kwa mujibu wa mtaalam Mgeni, hakuna aina ya uzazi wa mpango yenye ufanisi asilimia 100, bali kila mbinu ina faida na hasara zake.

Hapo anataja mambo mengi ya kuzingatia wakati wa kuchagua njia ya uzazi wa mpango katika ufanisi wake, gharama, urahisi wake kutumia au hatua ya mama mhusika kimaisha.

"Uzazi wa mpango wa kudumu kwa wanawake, unahusisha upasuaji wa kufunga mirija ya uzazi ili kuzuia mimba. Pia, wanaume wanaweza kupata uzazi wa mpango wa kudumu, unaoitwa 'vasektomi.'

Anasema ni hatua inyochukuliwa, pale mhusika anaweka dhamira ya kudumu ya kutotaka kupata ujamzito katika siku zijazo, lakini bado anasisitiza mbinu bora zaidi ni kuwa uzazi wa mpango wa kudumu.

### NJIA YA KINGA

Mgeni anafafanua kuna uzazi wa mpango wa dharura unaojulikana kama 'kidonge cha kesho asubuhi' ('morning after') unaotumika mhusika anaposahau kumeza kidonge, kama unafanya ngono bila kinga au kama kondomu inaharibika.

Anaongeza kwamba kidonge hicho huzuia au kuchelewesha utagaji yai, lakini sio daima kuzuia mimba, akifafanua kidonge cha dharura cha kuzuia mimba kinapatikana kutoka kwa daktari, pia vipo kwa Wafamasia madukani.

Kwa utendaji wake, Mgeni anasema kinafaa kwa wastani zaidi ya asilimia 85 na kina ufanisi hasa, kinapotumiwa ndani ya saa 24, baada ya kufanyika tendo la ndoa.

Vilevile mtaalam huyo, anaeleza kuwapo njia za uzazi wa mpango wa kisasa, ambazo utendaji wake unatofautiana, hivyo mwanamke huamua kutumia njia mojawapo ya uzazi wa mpango, kama ifuatavyo:

Mtaalamu huyo anataja; Vipandikizi vya Homoni vinafaa zaidi ya asilimia 99, daktari au muuguzi hukiweka kipandikizi hicho (implant) kidogo chini ya ngozi ya mkono wake wa juu.

Pia, anatoa homoni inayoitwa 'projestojeni', inayozuia utagaji mayai na kipandikizi hudumu kwa miaka mitatu.

Aidha, ipo njia ya kupigwa sindano za homoni inayotajwa inafaa kwa zaidi ya asilimia 96, ikitajwa daktari au muuguzi anampa mhitaji sindano ya homoni hiyo ya 'projestojeni' kila baada ya wiki 12, ambayo ni sawa na miezi mitatu.

Pia, anataja nyingine kinga aina ya IUD, inayofanya ufanisi zaidi ya asilimia 99. Hiyo inafanyika kwa kuingizwa kifaa kiitwacho 'IUD' (kifaa kidogo chenye umbo la T) kwenye mfuko wa uzazi kupitia sehemu ya uke, ikizuia mbegu kufika kwenye yai.

Hata hivyo, inatajwa kuwa ni njia hizo 'IUD' za shaba, zinadumu kwa miaka mitano hadi 10.

Vilevile, nyingine anaitaja kuwa kidonge kinachofanya kazi kwa ufanisi zaidi ya asilimia 93, inayomeza wakati huo wa tendo hilo kila siku, ikizuia ujauzito.

Kunatajwa kuwapo aina mbili kuu za uzazi wa mpango wa mdomo, mtaalam Mgeni akitaja kimoja ni kidonge cha pamoja cha uzazi wa mpango, ambacho kina homoni za 'estrojeni' na 'projestoroni.'

Pia, anasema kuna njia inayofahamika pete za uke, ambayo zina ufanisi zaidi ya asilimia 93. Anasema, huwa ina homoni sawa, ambazo ziko kwenye kidonge cha pamoja cha uzazi wa mpango.

Hiyo anataja kuwekwa pete mpya katika sehem ya uke kila mwezi na kuiacha hapo kwa wiki tatu, ili kuzuia mimba.

Anaeleza kuwapo njia inyojulikana kwa wengi, utumiaji kondomu, ikiwa nayo aina pekee ya uzazi wa mpango unaozuia pia maambukizi ya magonjwa ya zinaa (STI), akiitaja inaweza kutumika kwa pamoja na njia nyinginezo tajwa za uzazi wa mpango.

### USHAURI ULIOPO

Mtaalam Mgeni, anawashauri wanawake kutumia njia za uzazi wa mpango, kwani ina msaada mkubwa katika kufikia afya njema kwao, kupata muda mzuri wa kufanya maendeleo, pia mwanamke atautambua mzunguko wa hedhi vizuri na salama, haibadili homoni zao za mwili.

Hata hivyo, mtaalamu huyo anawaasa wanawake na wanaume, kuwa ni vyema wakazielewa njia zote za uzazi wa mpango kabla ya kutumia, ili wawe na uchaguzi sahihi.

"Ili apate huduma sahihi anapohitaji kuanza uzazi wa mpango, aende kwa mtoa huduma sahihi ambaye amesomea njia zote za uzazi wa mpango," anasema, pia akihitimisha:

"Ili kabla ya kupewa afanyiwe ushauri wa kina, aelewe kitakachotokea, na hatuiti madhara, tunaita 'maudhi madogo madogo'..."

## SIMULIZI WIMBI LA MATESO YA UZAZI, NDOA KWA WANAOLEA WENYE KIFAFA

**Inatoka Uk. 12**

### KUTOKA SERIKALI

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD's) na Afya ya Akili kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, anasema kunahitajika maboresho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, katika kifungu kinachoruhusu wanandoa kuachana iwapo kuna mmoja anaugua kifafa.

"Sikujua wakati huo walipotunga sheria hii kifungu hicho walikuwa na sababu gani, kunahitajika maboresho," anasema Dk. Ubuguyu, akaongeza:

"Tunafanya kazi na wanasheria kutoka TAWLA (Chama Cha Wanasheria Wanawake,) kuangalia sheria na sekta zingine ili kuboresha. Sheria hii ukiitazama hasa imeegemea sera, imani na si katika mambo mengine."

Anasema mkakati ni kuhakikisha vipimo na dawa iitwayo 'phenobabitol', inapatikana katika hospitali na vituo vya afya nchini kote.

"Ingawa kuna dawa nyingine zaidi ya hiyo, lakini angalau hiyo ya msingi ambayo inasaidia kwa asilimia 70 wagonjwa wa kifafa inawasaidia," anasema Dk. Ubuguyu.

Dk. Ubuguyu anasema kwamba, serikali ipo mbioni kukamilisha mpango wa Afya kwa Wote ambapo kila Mtanzania, yakiwamo makundi tofauti yatanufaika na huduma hiyo. "Sababu ya kifafa inaweza kuwa ajali, au katika hatua ya 'labour process' (michakato ya ajira) wakati wa kuzaliwa, ni sababu kubwa ya kuweka makovu kichwani.

"Tumefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua, lakini tunahitaji kumlinda mtoto pia eneo hili, ili kichwa kisiathiriwe," anasema.

AFYA

## PREECLAPMSIA

# Ugonjwa tata unaowatesa kinamama wazazi, ukiwapa kitendawili watafiti

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA ugonjwa tata wa Preeclampsia, unaotajwa kitaalamu kuwa ni janga linalosababisha vifo vya kinamama zaidi ya 70,000 kila mwaka, lakini sababu zake bado ni kitendawili kwa wanasayansi.

Inakadiriwa vifo vingi vikitokana na kiharusi au uzazi, kutokana na shinikizo la damu na kifo chake kinaweza kutokea bila tahadhari kwenye ujauzito.

Wapo wanawake wanaopata shida hiyo kabla ya wiki 34 za ujauzito na wengine katika hatua ya mwisho kuelekea kujifungua.

Wanasayansi wamegundua baadhi ya dalili zake zikianzia kuvimba sana tumboni, inaharibu mifumo ya mawasiliano kati ya mwili wa mama na kijusi.

Pia, inaathiri urekebishaji wa mishipa ya damu ndani ya tumbo la uzazi ili kulinda kondo, eneo ambalo husambazia kijusi (kichanga tumboni) virutubisho na hewa oksijeni inayohitajika.

Pia, kunakuwapo mtiririko wa damu usio wa kawaida kupitia kondo la nyuma, ambayo husaidia mwili wa mama kudhibiti shinikizo la damu, hatua kwa hatua husababisha shinikizo la damu na preeclampsia.

"Wakati wa ujauzito, moyo wa mama unapaswa kusukuma damu zaidi kwa mtoto na kondo. Kiasi cha damu inachosukuma kila dakika ni mara moja na nusu hadi mbili zaidi ya mimba ya kawaida," anasema Ian Wilkinson, Profesa wa Tiba, katika Chuo Kikuu cha Cambridge, anayeongoza watafiti wa Uingereza katika shida hiyo. Kuna hali zinazotajwa kuongeza hatari ya kupata maradhi 'preeclampsia'. Inatajwa ni pamoja na wanawake wanaougua kuwa na kinga ndogo na wajawazito wenye umri zaidi ya miaka 40.



Mzazi anayesadikiwa kuugua maradhi ya Preeclampsia, akipata matibabu na mwanawe mchanga. **PICHA: MTANADAO.**

Lingine linatajwa, ni kwa wanawake wenye uzito mkubwa, hawawezi kukabiliana na uzito wao unaoongezeka wakati wa ujauzito.

**INATAMBULIWAJE?**

Ingawa wataalamu wa magonjwa mengine kama vile saratani au maambukizi sugu wanaweza kuchukua vipimo vya tishu za ndani za mgonjwa kwa uchunguzi zaidi, bado kunatajwa hakuna njia rahisi ya kutambua mabadiliko yanayotokea kwenye tumbo la uzazi la mwanamke mjamzito.

"Hatuwezi kuchukua mara kwa mara sampuli ya kondo la mwanamke mjamzito, kwa sababu hiyo huongeza hatari ya kuharibika kwa mimba," anasema Lana McMullins, Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Teknolojia Sydney, Australia.

Anaendelea:"Na wanyama hawapati pre-eclampsia (wakati wa ujauzito), kwa hivyo kutumia mifano ya panya, kwa mfano, ni vigumu sana."

Kuna uchunguzi wa mwaka juzi, unaoonyesha namna chembehai zinavyoonyesha kondo kwa wanawake walio na viwango vya juu vya uvimbe kwenye tumbo la uzazi, huonyesha usambazaji dhaifu wa damu kwa kutoa protini inayojulikana kama tyrosine kinase 1 (sFlt-1).

"Protini hii huwa katika viwango takriban mara 100 zaidi ya kawaida kwa wagonjwa walio na preeclampsia," anasema Craig Mello, Profesa wa Baiolojia katika Chuo Kikuu cha Massachusetts, Uingereza na mshindi wa Tuzo ya Nobel 2006.

# Ilivyo safari yake Samia kitabibu, dhamana tiba mpya kwa wagonjwa

**Inatoka Uk. 11**

kuigharamia.

**KINACHOENDELEA KISEKTA**

Kwa ujumla, kinachoendelea katika vita vya maboresho katika Sekta ya Afya katika zama Awamu ya Sita yenye miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Rais Dk. Samia madarakani, ina mengi yanayoambata na nyenzo bima ya afya.

Ni wastani wa wiki moja sasa, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mnamo tarehe 21 iliyopita, amezindua Ripoti ya Mapitio ya Hali ya Utekelezaji wa Afya kwa Wote na Utayari wa Kukabiliana na Dharura Nchini, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Hapo akaahidi Serikali ya Muungano wa Tanzania, pia na ya Zanzibar, zitaendelea kushirikiana na wadau, pia taasisi za kiafya kuhakikisha huduma za afya zinaimarika, kukabiliana na dharura zake nchini.

Vilevile, Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, anasema, Serikali ya Rais Dk. Samia kwa kiasi kikubwa imechukua hatua kwa sekta afya, akitumia marejeo zaidi ya shilingi trilioni 6.2 zimetumika kuimarisha, ndani ya miaka mitatu sasa.

Anasema mtazamo uliopo kiserikali ni kwamba, hatua hiyo itakuwa mwarobaini unaowahakikishia Watanzania wananufaika na uwekezaji, wakipata huduma za afya wakiwamo walio na vipato duni. Hayo ni kutokana na jitihada za serikali kutenga fedha za kundi hilo.

Vilevile katika tukio lingine tarehe 19 mwezi huu jijini Dodoma, katika ufunguzi wa Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Afua Jumuishi za Kondomu, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono, Kaimu Mkuu wa Programu anayesimamia Ukimwi na magonjwa hayo tajwa, Dk. Kisonga Riziki, ana ufafanuzi wake.

Anasema, serikali imeazimia kuimarisha mnyororo wa ugavi na upatikanaji wa kondomu nchini, sambamba na kutoa elimu iwafikie wananchi wote mahitaji, ikiwamo pembezoni mwa nchi, katika maeneo ya miji midogo na wilayani.

"Tumeazimia kuimarisha juhudi zetu za kukuza matumizi sahihi na endelevu ya kondomu kwa kutoa elimu zaidi kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na elimu ya ana kwa ana.

"Ni muhimu kuelimisha jamii kuwa kondomu ni kinga dhidi ya VVU, magonjwa ya ngono, mimba zisizotarajiwa na pia ugonjwa wa homa ya ini," anasema Dk. Kisonga.

Anaendelea: "Tunazidi kuhakikisha kwamba kondomu zinapatikana na kufikiwa na watu wote, hasa katika maeneo ya pembezoni na ambayo hayana huduma ya kutosha, kuendelea kupenya zaidi katika maeneo ya miji midogo na wilaya ili kutanua soko.

"Kwa kipindi cha Januari 2023 hadi Oktoba 2024 Wizara imeagiza na kusambaza kondomu aina ya zana inayotolewa bila malipo kwa walengwa zipatazo171,665,200 zenye thamani ya Tsh. 14,014,217,787.19."





## BoT yataka mawakala benki wakusanye noti

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imezitaka benki za biashara kuwaelekeza mawakala wao kusaidia kuchukua noti za zamani zinazoondolewa kwenye mzunguko ili kuziwasilisha sehemu husika.

Zoezi la kuziondoa noti hizo limepangwa kuanza Januari 6 hadi Aprili 5, mwakani ambapo noti hizo hazitaruhusiwa kutumiwa na taasisi yoyote.

Meneja Huduma za Kifedha na Sarafu kutoka BoT, Nolasco Mallu, alisema hayo kwenye mkutano na waandishi wa habari pamoja na watu wa benki uliofanyika jijini.

Mallu, alisema wananchi wengi wa vijijini hawana nafasi ya kuzikaribia benki kwa ajili ya kuzirejesha fedha hizo, hivyo wao wanapaswa kuwaelekeza mawakala wao kuzipokea ili kuwasaidia wananchi kuepuka kukutana na madalali watakaojifanya wanatoka benki kwa ajili ya kukusanya noti hizo.

Alibainisha kuwa noti hizo zinazotakiwa kurejeshwa kuwa ni zile za Sh. 20, 200, 500, 1,000, 2,000, 5,000 na 10,000 za kuanzia mwaka 1985 hadi 2003 pamoja na ile ya Sh. 500 ya mwaka 2010, ambayo serikali ilifanyia mabadiliko kuwa sarafu.

Alisema sababu kubwa ya kuziondoa noti hizo ni pamoja na kuzunguka kwa jamii kwa muda mrefu jambo lililopeleka kuchakaa kwa muda mfupi.

Hata hivyo alizitaka benki kuwa makini katika suala zima la upokeaji noti hizo kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao watatumia nafasi hiyo kuleta noti feki na kuongeza kuwa wanapaswa kuzikagua.

Alisema ili kuwasaidia wananchi kuzitambua noti hizo benki za biashara mnapaswa kuwapokea ili kuwaepusha kukaa nazo na kupita muda ambao umepangwa na serikali kwa ajili ya kuziondoa katika mzunguko.

Pia, alizitaka benki kuwasaidia wananchi kuzitambua noti hizo ili kuepuka kutapeliwa na baadhi ya watu ambao hupenda kutumia fursa hizo kuwadanganya wananchi.

Naye Meneja Msaidizi wa Kitengo cha Sarafu, Matilda Luvinga, alizitaka benki kusaidia kuwapokea wateja wanaokuja na fedha hizo kuwabadilishia na wao kuziwasilisha BoT ndani ya muda uliopangwa.

# Wahadhiri, wanafunzi wapewa elimu ya ubunifu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewajengea uwezo kuhusu masuala ya usajili wa ubunifu mbalimbali wahadhiri na wanafunzi kutoka vyuo vikuu na ufundi mkoani Dodoma.

Akizungumza baada ya mafunzo hayo yaliyofanyika jijini hapa jana, Ofisa Usajili wa BRELA, Stanslaus Kigosi, alisema wanatoa elimu kuhusu miliki bunifu kwa sababu katika taasisi za elimu kuna utafiti na bunifu mbalimbali unafanyika zinahitaji kulindwa.

Msimamizi wa Kitengo cha Ujasiriamali na Ubunifu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Salum Matotola, alishukuru BRELA kwa kutoa mafunzo hayo kwa kuwa katika vyuo wanafanya utafiti lakini wanaishia kuyaweka matokeo husika katika maktaba badala ya kuwasilisha katika jamii.

Mhadhiri kutoka UDOM, Dk. Benta Matunga, alisema mafunzo hayo yamewawezesha kufahamu namna BRELA inavyofanya shughuli zake ikiwamo hatua za usajili wa shughuli za kitafiti na bidhaa mbalimbali.

Mhitimu kutoka UDOM, Sospeter Jonathan, alisema alianza kujishughulisha katika masuala ya kiubunifu tangu akiwa mwaka wa kwanza wa masomo lakini hakuwa akifahamu kuhusu usajili wa miliki bunifu.

# Serikali kuunganisha mtandao wa barabara vijijini, mikoa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete, amesema serikali inakusudia kuunganisha mtandao wa barabara kutoka vijijini, mikoa hadi miji mikuu.

Amesema lengo ni kuongeza tija kwa kurahisisha mawasiliano kwa wakulima kusafirisha bidhaa za vyakula na biashara.

Alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizindua mradi wa maboresho ya barabara za vijijini unaosimamiwa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

Ridhiwani alisema: Mradi ni mkubwa sana kama ambavyo mmesikia utakwenda kunufaisha asilimia kubwa ya wananchi wetu hasa wale wanaoishi maeneo ya pembezoni kwa sababu unakwenda kuongeza mtandao wa barabara zinazotoka vijijini ikiwamo kuimarisha usimamizi wake ambapo itafungua kwa wakulima na wafanyabiashara."

Alisema kuna watu wanalima lakini wanapata shida ya kufikisha mazao yao sokoni, hivyo mradi huo unakwenda kuunganisha barabara za vijijini, wilaya na mikoa.

"Kika mtu ana eneo lake la kusimamia, unakuja kuangalia namna gani barabara za vijijini zinakutana na barabara za mikoa. Hasa katika maeneo ya wakulima ambapo bidhaa zitakuwa zinachukuliwa kutoka katika vyama vya ushirika au maghala," alisema Ridhiwani.

Alisema mradi huo unakwenda kuendeleza uchumi wa nchi na wa mtu mmoja mmoja pamoja na kero zinazowakabili wakulima vijijini, kujenga uwezo, kuongeza ujuzi.

Ridhiwani alisema Rais Samia Suluhu Hassan tangu alipoingia madarakani ameongeza bajeti ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kutoka Sh. bilioni 250 hadi Sh. bilioni 850.

Alisema pia mtandao wa barabara umeongezeka na kufikia kilometa 3,337 kutoka lengo la kufikia kilometa 3,100 iliyopangwa ifikapo mwaka 2030.



Mkazi wa Mtaa wa Sokoine, Kijiji cha Chamwino Ikulu, mkoani Dodoma, Heleni Malecela, akipiga kura ya kuwachagua viongozi wa serikali za mitaa kijijini hapo jana .PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# IRDP yaanza utafiti sekta ya umwagiliaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), Prof. Hozen Mayaya, amesema chuo hicho kinafanya utafiti wa sekta ya umwagiliaji na uongezaji thamani kwenye zao la mpunga ili kuleta tija kwenye kilimo.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa, Prof. Mayaya alisema wanaamini utafiti huo utasaidia wizara kuwa na ubunifu nyingi za uboreshaji na uongezaji thamani wa mazao ya chakula.

Aidha, Prof. Mayaya alisema sekta ya kilimo inaigusa jamii moja kwa moja kutokana na wengi kutegemea kilimo ili kujiinua kiuchumi, hivyo wao kama chuo katika utafiti wanaofanya wamelenga kufanya kwenye kilimo kisaidie jamii.

Alisema lengo lao ni kuona kilimo kinakuwa na tija kwa taifa na jamii kuondokana na kilimo cha mazoea ili kuleta matokeo chanya.

Kadhalika, alisema moja ya mafanikio ya chuo hicho iliyopata ni kuongezeka kwa utafiti unaofadhiliwa na chuo hicho kutoka tafiti saba zenye thamani ya Sh.milioni 84 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 16 zenye thamani ya Sh.milioni 240 kwa mwaka 2022/23.

Alibainisha kuwa kumekuwa na utekelezaji wa miradi ya utafiti shirikishi kwa lengo la kujenga uwezo wa taasisi na watu binafsi ili kutatua kero za kiuchumi zinazoikabili jamii.

Alisema baada ya kufanya mapitio ya mitaala 15 na kuanzisha mingine saba, chuo kimekidhi mahitaji yanayotakiwa na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Mipango, Prof. Joseph Kuzilwa, aliishukuru serikali kwa kuwapatia jengo lenye miundombinu ya kisasa kutokana na ufadhili wa mradi wa mageuzi ya kiuchumi kupitia elimu ya juu.

Prof. Kuzilwa alisema hiyo inaonyesha jinsi gani serikali ilivyowekeza kwenye sekta ya elimu ili kuhakikisha chuo kinazalisha wataalam walio bora wanaokwenda kulisaidia taifa kutatua matatizo ya kimaendeleo.





# Watuhumiwa kumuua mtoto kisa kujisaidia kwenye nguo

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wawili ambao ni mume na mke kwa tuhuma za kumuua mtoto wao kwa kumcharaza bakora wakimtuhumu kujisaidia kwenye nguo

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Benjamin Kuzaga aliyasema hayo jana alipozungumza na wandishi wa habari ambapo aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ramadhan Mwakilasa (28) na Mariamu Mwashambwa (28).

Alisema watuhumiwa hao walimuua mtoto wao, Cloy Ramadhan (04) ambaye alikuwa mtoto wa kambo ambaye Ramadhan alizaa na mwanamke mwingine.

Alisema tukio hilo lilitokea Novemba 25 mwaka huu saa 2:00 usiku katika Mtaa wa TEKU viwandani jijini Mbeya ambapo watuhumiwa walimpiga na fimbo sehemu mbalimbali za mwili wake na kusababisha kifo chake.

"Uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha tukio hilo ni ukatili na unyanyasaji kwa kumuadhibu mtoto baada ya kujisaidia kwenye nguo alizokuwa amezivaa," alisema Kamanda Kuzaga.

Kamanda Kuzaga aliwataka wazazi na walezi kuacha vitendo vya kujichukulia sheria mkononi dhidi ya watoto pindi wanapokosea na badala yake watumie njia sahihi na salama kuwafundisha au kuwaelekeza bila kusababisha madhara.

Watu hao wametenda ukatili huo dhidi ya mtoto wao ikiwa ni ndani ya kipindi cha siku 16 za kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto duniani.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akiangalia alama ya wino kwenye kidole cha wapigakura wenzake inayoonesha kuwa amepiga kura jana, kwenye kituo cha Shule ya Msingi Umoja ya jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maambukizi VVU Songea yapungua kwa 0.7%

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

HALI ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) imepungua kutoka asilimia 5.6 mwaka 2016/2017 hadi kufikia asilimia 4.9 mwaka 2023 sawa na asilimia 0.7 ya kiwango kilichopungua.

Hayo yalielezwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahamed Abbas wakati akizindua maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani katika viwanja vya Majimaji ambayo kitaifa yanafanyika mkoani Ruvuma.

Alisema katika maadhimisho hayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema kuwa kuhusu hali ya UKIMWI mkoani Ruvuma takwimu zinaeleza kuwa wanaoishi na maambukizi ya VVU wapo 68,237 kati yao wanaume ni 24,959 sawa na asilimia 37, wanawake 43,000 sawa na asilimia 63.

Watoto chini ya umri wa miaka 15 wapo 2,382 sawa na asilimia 3.5 na watu wazima kuanzia umri wa miaka 15 wapo 65,855 sawa na asilimia 96.5.

"Ndugu viongozi pamoja na wananchi halmashauri zetu zinazoongoza ni Manispaa ya Songea ikifuatiwa na Tunduru lakini vile vile na Halmashauri ya Mbinga, hivyo napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote kuzingatia tiba na matunzo lakini vile vile kuendelea kutumia dawa za kufubaza," alisema Kanali Ahamed.

Kwa upande wake mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dk. Catherine Joachim aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na wananchi wake kwa kupiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa ushamiri wa VVU umeshuka kutoka asilimia 5.6 mwaka 2016/17 mpaka asilimia 4.9 mwaka 2022.

Alisema kuwa takwimu hizo zinaonesha Mkoa wa Ruvuma unaongoza katika upimaji wa VVU hata hivyo umeendelea kufanya vizuri katika VVU vya 95/95/95 ambapo ushamiri wa utafiti wa mwaka 2023 tumeonesha asilimia 82 ya wananchi wanatambua hali zao za maambukizi.

Alisema asilimia 97 ya walioambukizwa wanatumia dawa za kufubaza VVU na asilimia 99 ya wanaotumia dawa za kufubaza tayari wameshafubaza virusi jambo ambalo linaoneaha mkoa huo umepiga hatua kubwa sana ikilinganishwa na mwaka 2016/17.

"Japokuwa mkoa upo nyuma ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa 95/95/95 ambapo 95 ya kwanza kitaifa tupo asilimia 83, 95 ya pili tupo asilimia 98 na 95 ya tatu tupo asilimia 94" alisema Dk. Catherine.

Alieleza zaidi kuwa kutokana na Mkoa wa Ruvuma umeendelea kukua kiuchumi kupitia shughuli za kilimo,migodi ya makaa ya mawe na madini mengine, usafirishaji na uvuvi maendeleo hayo yamepelekea nakisi kubwa kwenye usawa unaopelekea baadhi ya makundi kuwa katika hatari zaidi ya maambukizi ya VVU.

Mwakilishi wa Baraza la Watu Wanaoishi na VVU na Mwenyekiti wa Shirika la NACOPHA, Letisia Moris alisema kuwa hali ya unyanyapaa na ubaguzi wa VVU bado ni changamoto ndani ya jamii hivyo utaathiri juhudi za kutokomeza UKIMWI wakati ni sawa kwa kila mmoja kuzingatia kaulimbiu ya mwaka huu.

## Wakazi Mbeya vinara matumizi ya mkaa kupikia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JIJI la Mbeya limetajwa miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wake wanatumia kiwango kikubwa cha mkaa kwa ajili ya kupikia, hali ambayo inachangia uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa misitu katika maeneo mbalimbali.

Kamishna Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (CC), Prof. Dos Santos Silayo aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya ikiwemo kwenye vyanzo vya maji na kwenye taasisi za elimu.

Alisema takwimu zilizopo ni kwamba wananchi wa Jiji hilo wanatumia kiwango kikubwa cha mkaa ambao unachomwa katika Wilaya za Chunya, Songwe na maeneo mengine ya jirani.

Aliwataka wananchi wa Jiji hilo kubadilika na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo gesi ili kupunguza kiwango cha uharibifu wa mazingira kwenye maeneo hayo pamoja na kulinda afya za wananchi.

Alisema uharibifu huo wa mazingira unasababisha mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kupungua kwa kiwango cha mvua na kuongezeka kwa joto duniani.

Aliipongeza taasisi ya Tulia Trust ambayo inaongozwa na Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson kwa kujitolea miti hiyo ambayo itapandwa kwenye maeneo mbalimbali kwa lengo la kulinda mazingira.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Dk. Tulia alisema taasisi yake ilianza kutoa miti hiyo zaidi ya miaka miwili iliyopita ambapo ilianza na miti ya matunda ambayo ilikuwa inatolewa bure kwa wananchi kwa ajili ya kupanda kwenye makazi yao.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kupanda zaidi ya miti 2,000,000 na kwamba kwa mwaka huu wanatarajia kupanda miti 2,000 kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye vyanzo vya maji na kwenye shule mbalimbali za msingi na sekondari.

Alisema mbali na maeneo hayo pia watapanda miti hiyo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na maeneo yote ya wazi ili kuhakikisha yanakuwa salama.

Aliwataka wadau wengine wa mazingira kushiriki katika kupanda miti kwenye maeneo yote ya wazi ili kuhakikisha maeneo yote ya wazi yanakuwa safi.

Diwani wa Kata ya Mwakibete ambako upandaji huo wa miti ulizinduliwa, Lucas Mwampiki alisema watahakikisha wanalinda miti hiyo ili istawi na kutimiza azma ya serikali.

Pia, aliwataka wananchi wa kata hiyo kushiriki kwenye upandaji wa miti na kuitunza na kwamba kila mwananchi anatakiwa kushiriki kuipanda na kuitunza ili istawi.



## Serikali yaanza kukomesha vitendo vya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imesema imeanza kuchukua hatua ya kukomesha vitendo vya udhalilishaji.

Imesema kufanikisha hilo inashirikiana na Jeshi la Polisi na madawati ya jinsia kutoa elimu inayohusiana na watoto juu ya namna ya kujikinga dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto.

Waziri wa wizara hiyo, Tabia Mauli Mwita aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe Ameir Abdallah Ameir.

Ameir alitaka kujua wizara inachukua jitihada zipi katika kukomesha vitendo hivyo kwa watoto na pia ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa makocha na viongozi waliohusika kuwadhalilisha watoto kwenye tasnia ya michezo.

Akijibu swali hilo, Tabia alisema pia wizara yake ikichukua hatua kali kwa wale wanaobainika kufanya vitendo vya udhalilishaji wa watoto katika michezo.

"Mheshimiwa Spika, suala la udhalilishaji kwa watoto ni jambo ambalo halikubaliki katika michezo, endapo kiongozi, kocha au mchezaji atakayebainika ana tabia kama hizi Wizara inachukua hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema.

Alisema kwa mujibu wa kanuni za michezo ikibainika hufungiwa moja kwa moja katika maswala ya michezo.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul alikiri kwamba kuna ongezeko la vituo vya kulea watoto vya binafsi ambapo mwaka 2020 kulikuwa na vituo tisa lakini kwa sasa kuna vituo 17.

Alisema hayo wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Muhammed Ali Suleiman aliyetaka kujua kuna vituo vingapi vya watu binafsi vya kulea yatima Zanzibar vimepata usajili.

Alisema kati ya vituo hivyo, 12 vimeshapatiwa usajili na vitano bado, kwamba taratibu za kukamilisha usajili haujakamilika.

Alisema Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuhamasisha jamii kuhusu watoto kulelewa kwenye familia zao na kuacha kuanzisha vituo kiholela.

Alisema jamii inaendelea kuwasaidia watoto yatima kwa kushirikiana na Wizara kwa kukabali kujiunga na programu mbalimbali zinazolenga kuwalea watoto yatima.

Alisema pia wanajamii hutoa misaada mbalimbali ya kifedha na vifaa vya mahitaji ya msingi kwa watoto hao na wizara inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba watoto waliopo vituoni wanaungana tena na familia zao za asili.

# BoT: Kuondoa fedha za zamani kutadhibiti uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema kuwa kutoa fedha mpya na kuondoa za zamani kutasaidia kudhibiti matukio ya uhalifu.

Mkurugenzi wa BoT tawi la Zanzibar, Ibrahim Malogoi, alisema hayo juzi wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari Zanzibar yaliyohusu ubadilishaji wa fedha za zamani na kuziondoa katika mzunguko.

Alisema kuna fedha zilizotolewa mwaka 1985 zipo katika mzunguko, hivyo wajibu wa BoT ni kutengeneza fedha na kuzitoa kwa ajili ya kurahisisha biashara na mabadilishano ya huduma.

"Baada ya muda mwenye jukumu la kuziondoa fedha au kuziharibu ni BoT na hili ni jukumu la kisheria kwa hiyo tumeamua sasa kuziondoa fedha za tangu mwaka 1985 mpaka mwaka 2003 kwa baadhi ya fedha" alisema.

Aidha, alisema BoT pia itaiondoa fedha ya noti ya Sh. 500 kwenye mzunguko ambayo ni ya mwaka 2010 ambapo benki hiyo imeshatengeneza sarafu ya fedha hiyo.

Alisema fedha hizo hazihara-mishwi, hivyo mtu akikamatwa na fedha hizo hatakuwa na mashtaka bali itakuwa hazitumiki tena na itakuwa ni kama kumbukumbu.

Alisema zoezi hilo la kuondoa fedha za zamani za tangu mwaka 1985 hadi 2003 litafanyika kwa muda wa miezi minne na ukomo wake ni Aprili mwakani.

Alisema faida ya zoezi hilo la kuondoa fedha ni kudhibiti utengenezaji wa fedha bandia, kufanya makadirio sahihi ya uchumi na kuondoka na upotoshaji.

Meneja Msaidizi Kitengo cha Sarafu BoT, Zanzibar, Suleiman Khalfani Rajab, alisema zoezi la kuziondoa fedha za zamani lipo kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 20006, Kifungu cha 28 ambacho kinaipa nguvu ya kuiondolea thamani fedha ambayo imeitangaza.

Alisema kwa ajili ya kuondoa mkanganyiko kwa jamii BoT imedhamiria kuondoa fedha za zamani, hivyo wananchi wasiwe na hofu.

Aidha, alisema hakutakua na changamoto itakayopatikana katika uchumi kutokana na zoezi hilo la kubadilisha fedha za zamani.

Baadhi ya waandishi wa habari waliopatiwa elimu hiyo, walisema watahakikisha elimu waliyoipata wataifikisha kwa jamii ili kufahamu lengo la zoezi hilo la ubadilishaji wa fedha.

Mwandishi wa habari wa ITV, Farouk Karim alisema suala la fedha ni muhimu sana katika nchi na bila ya kutoa taaluma, wananchi watapoteza fedha zao bila ya sababu.

Katibu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) Mwinyimvua Abdi Nzukwi, alisema waandishi wa habari ni daraja la kuwafikia wananchi.



Meneja msaidizi kitengo cha sarafu kutoka Benki kuu Tanzania (BOT) Ofisi ya Zanzibar, Suleiman Khalfani Rajab akitoa elimu kwa waandishi wa habari visiwani Zanzibar kuhusu zoezi la ubadilishaji wa fedha za zamani kutoka mwaka 1985 hadi mwaka 20003 zoezi ambalo litaanza Januari hadi April mwaka 2025. **PICHA RAHMA SULEIMAN**

## Sheria ya madini kufumuliwa, kusukwa upya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar imeanza maandalizi ya kuanzisha sheria mpya ya madini ili kuhakikisha rasilimali hiyo inawanufaisha wananchi na kuchangia zaidi katika uchumi wa Zanzibar.

Mkurugenzi wa Nishati na Madini kutoka wizara hiyo, Said Haji Mdungi, alisema hayo wakati akifungua mafunzo kwa wakuu wa wilaya na viongozi wa halmashauri na manispaa.

Alisema kuwa wizara imeona ipo haja ya kuwepo kwa sheria hiyo kwa sababu hivi karibuni kumefanyika utafiti na kuonekana kuwa Zanzibar kuna baadhi ya madini chini ya ardhi.

Alisema kuwa sheria hiyo inakwenda kutoa nafasi ya kuona vipi madini na rasilimali nyingine zinapata sheria inayojitegemea katika sekta hiyo, hivyo aliwataka viongozi hao kuwa weledi katika jambo hilo.

Alisema kuwa sheria hiyo itapelekwa kwa wadau ili kutoa maoni yao kwa faida ya watu wote.

Mdungi alisema sheria hiyo inalenga kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini kwa kudhibiti uchimbaji, usafirishaji, na utoroshaji wa madini kinyume cha sheria.

Akitoa mada katika mafunzo hayo mwanasheria kutoka wizara hiyo, Mhammed, alisema kuwa wakuu wa wilaya kwa mujibu wa sheria, ndiyo viongozi wakuu katika kamati zao za ulinzi na usalama za wilaya.

Alisema wanawajibu wa kusimamia ipasavyo sheria zilizopo za rasilimali zisizorejesha katika maendeleo hayo.

Aidha, alisema kuwa wizara inafahamu sheria zilizopo kwa sasa zimepitwa na wakati lakini mpango wa kuzibadilisha unafanyika ili kuendana na wakati uliopo hivi sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Othman Ali Maulid, alisema watakuwa mabalozi wazuri katika kuwaelimisha wananchi na kusimamia ipasavyo kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Wilaya wa Kaskazini A Unguja, Rashid Simai Msaraka alisema kuwa anamini rasilimali hizo ni muhumu, ataendelea kukaa na vijana kuwaeleza kwa sababu ndiyo walengwa wakubwa wa jambo hilo.

# HABARI PICHANI



Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, akipiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa Dar es Salaam jana, Mtaa wa Kambangwa, Kata ya Mwananyamala. **PICHA: IMANI NATHANIEL**




Baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Tunduma Road katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakiwa kwenye mstari wakisubiri kupiga kura za kuwachagua viongozi wa Serikali za Mitaa kwenye kituo cha Shule ya Msingi Mapelele. **PICHA: NEBART MSOKWA**




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, akipiga kura jana katika kituo cha kupigia kura ofisi za Ofisa Mtendaji wa Kata ya Misigiri, wilayani Iramba mkoani Singida. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Wananchi wakitafuta majina yao ili wapige kura ya kuchagua viongozi wa Serikali ya Mtaa katika kituo cha kupigia kura Rilling Station, Karume, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



.Mwenyekiti wa Tume ya Ulinzi na Taarifa Binafsi na Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Muheza, Tanga, Balozi Adadi Rajabu (wa pili kushoto), akiangalia jina lake katika daftari la mkazi ili kupiga kura katika kituo cha Mkunguni, Kata ya Majengo wilayani Muheza jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Sokoine Kijiji cha Chamwino Ikulu, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, wakiwa kwenye foleni ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

HABARIKIMATAIFA

# Dawa ya pumu yahusishwa hatari afya akili

## • FDA yatahadharisha



Mfano wa namna ambavyo ugonjwa wa pumu unavyoathiri mfumo wa hewa kuelekea kwenye mapafu ya binadamu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Maulid Mmbaga**

WATAFITI wa serikali ya Marekani wamegundua kuwa dawa ya pumu inayotumika nchini humo ambayo awali iliuzwa na kampuni ya Merck inaweza kuhusishwa na matatizo makubwa ya afya ya akili kwa baadhi ya wagonjwa.

Kwa mujibu wa wasilisho la kisayansi lililotolewa siku chache zilizopita, watafiti waligundua kuwa dawa hiyo, inayouzwa chini ya jina la chapa ya 'Singulair' na kwa ujumla kama 'montelukast' inashikamana na vipokezi vingi vya ubongo muhimu kwa utendaji kazi wa akili.

Wasilisho hilo lililopitiwa na Reuters, linaeleza kuwa Singulair ilikuwa bidhaa ya kuvutia zaidi kwa Merck baada ya kuzinduliwa mwaka wa 1998, ikitoa unafuu katika kidonge kama mbadala wa kivuta pumzi.

Katika matangazo ya hivi karibuni, kampuni hiyo inasema madhara yalikuwa mabaya sana na kwamba yalikuwa sawa na kidonge cha sukari, huku lebo hiyo ikisema usambazaji wowote katika ubongo ulikuwa mdogo, na matoleo ya jumla bado yameagizwa kwa mamilioni ya watu wazima na watoto kila mwaka.

Inaelezwa kuwa hadi kufikia 2019, maelfu ya ripoti za matukio ya 'neuropsychiatric' pamoja na kadhaa ya kujiua, kwa wagonjwa walioagiziwa dawa hiyo walikuwa wamerundikana kwenye vikao vya mtandao na katika mfumo wa ufuatiliaji wa Utawala wa Chakula na Dawa wa Merika.

Wanasayansi wanaeleza kuwa ripoti kama hizo za matukio ya kutiliwa mashaka hazithibitishi moja kwa moja kiungo cha sababu kati ya dawa na athari, lakini hutumiwa na Kituo cha Kitaifa cha Utafiti wa Sumu (FDA) kubaini ikiwa uchunguzi zaidi wa hatari za dawa hizo unastahili.

Baada ya uchanganuzi wa miaka mingi, ripoti na utafiti mpya wa kisayansi ulisababisha mwaka 2020 FDA kuongeza onyo juu ya maagizo ya montelukast, ikiashiria hatari kubwa za afya ya akili kama vile kufikiria au vitendo vya kujiua.

Waraka huo pia uliitisha kundi la wataalamu wa ndani wakati huo huo ili kuangalia ni kwa nini dawa hiyo inaweza kusababisha athari za afya ya akili.

Inaelezwa kuwa matokeo ya kazi ya kikundi hicho, ambayo ni ya awali na hayajaripotiwa hapo awali au kutolewa hadharani, yaliwasilishwa kwa hadhira ndogo katika mkutano wa Chuo cha Marekani cha Toxicology huko Austin, Texas siku ya Jumatano.

Jessica Oliphant, Naibu Mkurugenzi wa FDA, anasema kwamba vipimo vya maabara vilionyesha kukinzana kwa kiasi kikubwa na 'montelukast' kwa vipokezi vingi vinavyopatikana kwenye ubongo.

FDA pia inathibitisha utafiti wa awali wa kisayansi unaoonyesha 'montelukast' kwamba hupenya pia kwenye akili za panya.

"Utafiti zaidi unahitajika kuhusu jinsi dawa hujilimbikiza katika mfumo wa neva, Oliphant. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa 'montelukast' ni ya juu zaidi katika maeneo ya ubongo inayojulikana kuhusika katika athari za akili," amesema.

Kwa mujibu wa data iliyotolewa kwenye wasilisho hilo, FDA haina mpango wa kusasisha lebo ya dawa hiyo.

**UTAFITI WAENDELEA**

FDA inatahadharisha kuwa tafiti zake zinaendelea, na matokeo hayajakamilishwa, baada ya kubaini kwamba tabia ya 'montelukast' inaonekana kuwa sawa na dawa zingine zinazojulikana kuwa na athari za afya ya akili, kama vile risperidone ya antipsychotic.

Wanasayansi Julia Marschallinger na Ludwig Aigner kutoka Taasisi ya Austria ya Tiba ya Kurekebisha Mishipa, wameiambia Reuters kwamba data mpya ilionyesha idadi kubwa ya 'montelukast' iliyopo kwenye ubongo.

Pia wanasema utafiti hauonyeshi ikiwa utaratibu huo unaongoza moja kwa moja kwa madhara kwa wagonjwa binafsi, au ni nani aliye hatarini, huku Marschallinger akisema data hizo mpya zinasaidia ripoti kutoka kwa watu walioripoti kuteseka na madhara.

Hata hivyo, kampuni ya Merck ambayo sasa inauza Singulair, inasema katika taarifa kwamba ina uhakika na wasifu wa usalama wa dawa hiyo.

"Lebo ya bidhaa ya Singulair ina taarifa zinazofaa kuhusu faida za Singulair, hatari na taarifa za athari mbaya," kampuni hiyo imesema.

Reuters iliripoti mwaka jana kwamba FDA ilipokea maelfu ya ripoti za wagonjwa, ikiwa ni pamoja na watoto wengi, wanaopata mfadhaiko, mawazo ya kujiua na tabia, au matatizo mengine ya akili baada ya kuanza kutumia dawa hiyo ya 'montelukast'.

Kufikia 2019, FDA ilijumlisha watu 82 waliojiua waliohusishwa na Singulair na matoleo yake ya kawaida yaliripotiwa kwenye hifadhi data yake ya matukio mabaya tangu 1998. Na kwamba angalau ripoti 31 kati ya hizo zilihusisha mtu aliye na umri wa miaka 19 au chini zaidi.

Vile vile, inaeleza kuwa mtoto wa kiume wa Robert Nick mwenye umri wa miaka 22 alijiua mwaka 2017 chini ya wiki mbili baada ya kuanza kutumia 'montelukast'.

Mzazi wa mtoto huyo anaeleza kuwa mtoto wake alikuwa na shida ya kulala kabla ya kufa na kwamba alikuwa mzima wa afya na hakuwa na matatizo ya akili kabla ya kutumia dawa hiyo.

"Alikuwa akitumia dawa hiyo kwa siku chache tu. Lakini ilibadilisha kabisa mwelekeo wa maisha yetu," amesema Nick.

Ripoti ya Reuters pia inaeleza kwa kina kesi zinazodai kuwa Merck ilijua kutokana na utafiti wake wa awali kwamba dawa hiyo inaweza kuathiri ubongo na kupunguza uwezekano wa matatizo ya akili katika taarifa kwa wadhibiti na kwamba nyingi za kesi hizo bado hazijakamilika.

**KUHUSU PUMU**

Pumu au Asthma ni ugonjwa unaothiri njia za hewa ambazo huingiza na kutoa hewa katika mapafu. Pia ni mojawapo ya magonjwa yasiyoambukiza, na kwamba huathiri takriban watu milioni 235 duniani, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Inaelezwa kuwa mtu mwenye ugonjwa huo kuta zake za ndani za njia ya hewa hupata maumivu ambayo kitaalamu huitwa 'inflammation' na kuvimba, na kwamba maumivu katika njia za hewa huzifanya njia hizo za hewa kujihami kwa kusinyaa na hivyo kupunguza kiasi cha hewa kinachopita kwenda kwenye mapafu.

***Chanzo Reuters***

# FOUNTAIN GATE YAMWEKA SOKONI KINARA WA MABAO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate imemweka sokoni straika wake tegemeo, Selemani Mwalimu, ambaye anaongoza katika orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Meneja Mwajiri wa klabu hiyo, Muhibu Kanu, amesema kiasi hicho wako tayari kumwachia straika huyo kwa dau la Dola za Marekani 400,000 sawa na zaidi ya Sh. bilioni moja za Kitanzania.

Kanu alisema kiasi hicho ndio thamani halisi ya mchezaji huyo ambaye anaongoza kwa kufumania nyavu kwa sasa katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaendelea tena kuanzia leo.

"Katika mkataba wake Mwalimu kuna kipengele kinasema anaweza kununua mkataba wake kwa Dola za Marekani 400,000 ambazo ni sawa na Sh. Bilioni Moja ya Kitanzania, klabu yoyote itakayotimiza hayo, tutafanya nao biashara hatuwezi kumzuia," alisema Kanu.

Kutokana na umahiri wake wa kupachika mipira ndani ya wavu, akiongoza katika orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akipachika jumla ya magoli sita, tayari klabu kadhaa zimeshaanza 'kummezea mate' straika huyo.

Straika hiyo amefunga mabao matano kwa mguu wa kulia na moja kwa kutumia mguu wake wa kushoto.

Alifunga kwa mguu wa kulia, ni katika mechi dhidi ya Namungo, timu yake ikishinda mabao 2-0, Dodoma Jiji zikitoka sare ya mabao 2-2, Kagera Sugar akiiongoza timu yake kushinda mabao 3-1, dhidi ya Prisons, ikipiteza mabao 3-2 na KMC, Fountain Gate ikishinda mabao 3-1.

Bao moja alilolifunga kwa mguu wa kushoto lilikuwa katika mchezo dhidi ya Ken-Gold, timu yake ikishinda mabao 2-1.

Alisajiliwa na Fountain Gate akitokea KVZ inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, ambapo msimu uliopita alikuwa mfungaji bora wa ligi hiyo, akipachika mabao 20.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Fountain Gate yenye pointi 17 baada ya kucheza michezo 11, iko kwenye nafasi ya saba.

Simba yenye pointi 28 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Azam yenye pointi 24 sawa na mabingwa watetezi, Yanga na Singida Black Stars inayokamilisha 'Top Four'.

Timu iliyopanda daraja msimu huu, Ken-Gold yenye pointi sita inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha klabu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

# Mtibwa Sugar, Geita vitani Championship

**Na Adam Fungamwango**

USHINDANI wa kutaka kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa timu zilizoshuka msimu uliopita, Mtibwa Sugar na Geita Gold umeendelea tena baada ya kila moja kushinda mechi zao za Ligi ya Champioship zilizochezwa hapo juzi.

Mtibwa Sugar wao walikuwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha, ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya TMA.

Mabao ya Mtibwa Sugar katika mechi hiyo yaliwekwa wavuni na Fredrick Magata dakika ya 19, na Anuary Jabir (dakika ya 69), huku Abdulaziz Shahame akiifungia TMA bao la kufutia machozi kwa penalti dakika ya 60.

Geita Gold ambayo nayo ilishuka daraja msimu uliopita, ilipata ushindi wa mabao 2-1, ikicheza ugenini kwenye Uwanja wa Mabatini ulioko Mlandizi mkoani, Pwani dhidi ya Cosmopolitan.

Malulu Thomas aliifungia Geita Gold bao la kwanza, Andrew Simchimba akipachika la pili wakati William Chang'a, akiifungia Cosmopolitan bao la kufutia machozi.

Matokeo ya mechi hizo imezifanya timu hizo zote kufikisha pointi 23 kwa michezo 10 ambayo kila timu imecheza, lakini Mtibwa Sugar inaongoza ligi hiyo ikiwa ikiwa na mabao mengi ya kufunga, ikipachika mabao 17, huku Geita Gold ikifunga mabao 13, na kushika nafasi ya pili ya msimamo, kila timu ikiwa imeruhusu mabao matano.

Timu hizo zimeweka wigo ya pointi nne kwa timu zinazowakimbiza, ambapo ni Songea United iliyoko katika nafasi ya tatu ikifuatiwa na Mbeya City wakati Stand United ikiwa nafasi ya tano, kila moja ikiwa na pointi 19.

Mbeya City na Stand United ambazo pia ziliwahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara miaka ya nyuma zenyewe zimetoka sare ya mabao 3-3 katika mchezo wa uliofanyika kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani, Shinyanga juzi.

Mabao ya wageni, yalifungwa na Pilla Pilla, dakika ya 45 na Malack Joseph, dakika ya 62 na 66, Tatizo Shem, Paschal Peter na Ally Hamis wakiwafungia Stand United mabao yao.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika hivi karibuni nchini Uganda. **PICHA: TFF**

# Zimamoto yapania makubwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Zimamoto SC imesema hakuna kitakachowazuia kutimiza mipango yao ya kumaliza katika nafasi ya nne za juu kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar, imeelezwa.

Zimamoto imetoa kauli hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mwenge SC katika mechi yake ya raundi ya 13 Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi.

Kwa sasa Zimamoto imefikisha pointi 21 na kukwaa hadi nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo sawa na KVZ FC walioko juu yao.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zima moto, Mohamed Hilali 'Tedi ' alisema amekipanga vyema kikosi chake ili kuhakikisha wanashinda michezo miwili iliyobaki ya mzunguko wa kwanza.**

Tedi alisema wamefanikiwa kufanya vizuri katika mechi tatu mfululizo na matokeo hayo yameendelea kuwahamasisha wachezaji wake kumaliza mzunguko kwa ushindi.

"Hamasa kwa wachezaji ndio kitu kikubwa katika kufanikisha lengo la ushindi, wanacheza kwa kujituma ili kuhakikisha mpango unafanikiwa, nina matumaini makubwa na wachezaji wangu katika kufanikisha mpango huu," Tedi alisema.

Aliongeza mechi hiyo dhidi ya Mwenge ilikuwa ngumu lakini juhudi za wachezaji wake zilisaidia kuondoka na pointi tatu muhimu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMUUZA ZIRKZEE

KLABU ya Manchester United inafikiria kumuuza, Joshua Zirkzee, miezi sita tu baada ya kumsajili huku Juventus ikimtaka mshambuliaji huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 23. ***(Corriere Dello Sport)***

### KVARATSKHELIA SOKONI

NAPOLI ipo tayari kumuuza Khvicha Kvaratskhelia msimu huu wa joto ikiwa mshambuliaji huyo wa Georgia hatasaini mkataba mpya, huku Manchester United wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Sportmediaset)***

### AMORIM ATUMA MASKAUTI

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim ametuma maskauti kumtazama winga wa Timu ya Taifa ya Ureno, Geovany Quenda mwenye umri wa miaka 26, mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres na winga wa Ureno, Pedro Goncalves (26), walipoichezea Sporting dhidi ya Arsenal juzi usiku. ***(Mail)***

### PORRO AKARIBIA MADRID

KLABU ya Real Madrid inataka kumsajili beki mpya wa kulia na kumwona mlinzi wa Tottenham Hotspur, Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 25 kama shabaha inayowezekana. ***(Sport)***

### FERGUSON NJIA MOJA

KLABU ya Brighton imemfanya mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, mwenye umri wa miaka 20 kupatikana kwa mkopo katika dirisha la Januari. ***(Telegraph)***

### UNITED YASAKA MLINZI

KLABU ya Manchester United inataka kusajili beki mpya wa kushoto msimu huu wa joto, huku wakiwawania beki wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 24 kutoka Canada, Alphonso Davies na mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa na AC Milan, Theo Hernandez (27). ***{Sports)***

### NISTERLROOY KUREJEA

RUUD van Nistelrooy mwenye umri wa miaka 48, ameivutia zaidi timu ya Leicester City baada ya kufanya mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### NWANERI MAMBO SAFI

ARSENAL ipo katika mazungumzo na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Ethan Nwaneri, mwenye umri wa miaka 17 kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu. ***(Fabrizio Romano)***

### OBI-MARTIN KIMEELEWEKA

KLABU ya Manchester United inatayarisha mkataba mpya kwa mshambuliaji Chido Obi-Martin wa Denmark atakapofikisha umri wa miaka 17 mwishoni mwa mwezi huu. ***(Tipsbladet)***

### EBOUE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inatazamia kumsajili kiungo wa kati wa Watford na Timu ya Taifa ya England, Mathis Eboue, mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni mtoto wa beki wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Eboue. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI AWAFIKIA RONALDO, MESSI ULAYA

●●● Ni baada ya kufikisha mabao 100 katika michuano hiyo huku...

**BARCELONA, Hispania**

ROBERT Lewandowski ameifikia rekodi ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kama wachezaji pekee katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufikisha mabao 100 au zaidi.

Lewandowski alifunga bao la 100 kwa penalti wakati Barcelona ikipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Brest na kuwawezesha kutinga nafasi ya pili katika muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Poland aliongeza bao la 101 katika kipindi cha pili.

Ronaldo anaongoza orodha ya wafungaji wa muda wote kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao 140, na Messi anafuata akiwa na mabao 129.

Lakini si Ronaldo wala Messi anayecheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sasa baada ya wawili hao kuhamia Saudi Pro League na MLS.

"Nina furaha sana, ni namba nzuri kuibua. Miaka iliyopita sikufikiri ningeweza kufunga zaidi ya mabao 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kujiunga na Messi na Ronaldo ... nadhani wako vizuri," alisema Lewandowski akiiambia Movistar.

"Kwangu mimi jambo la muhimu zaidi ni kujaribu kushinda kila mchezo, ikiwa naweza kufunga, basi hilo ndilo suluhisho kamili," aliongeza.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 36, alihitaji mechi 125 kufikia mabao hayo, mbili zaidi ya Messi (123) na 12 chini ya Ronaldo (137).

Kocha wa Barca Hansi Flick, ambaye pia alifanya kazi na Lewandowski katika klabu ya Bayern Munich, alisifu mafanikio ya mshambuliaji huyo.

"Ninamfahamu pia miaka miwili kutoka Munich; huko pia alivunja kila rekodi. Sasa anafunga pia. Ni muhimu kwetu. Lakini timu nzima inamuunga mkono. Wachezaji wengine watamsaidia kufunga mabao," alisema Flick.

Barcelona pia walipata bao katika kipindi cha pili kutoka kwa Dani Olmo na kurejea katika njia ya ushindi kufuatia mechi mbili za LaLiga bila ushindi.

"Nimefurahi sana kwamba tumeshinda leo (juzi) na kupata pointi tatu, lakini pia kwamba tulitawala mechi na mpinzani, alilinda vyema na kushambulia vyema," aliongeza Flick.

# Arteta atamba na ushindi wa kihistoria

**LISBON, Ureno**

MIKEL Arteta amesema ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Sporting CP ni "ushindi wa kihistoria" na uchezaji bora zaidi wa ugenini katika michuano ya Ulaya katika kipindi chake cha miaka mitano kama Kocha wa Arsenal.



Hapo awali Sporting hawakupoteza katika mechi 19 kwenye michuano yote msimu huu, lakini walifungwa kwa mabao ya Gabriel Martinelli, Kai Havertz, Gabriel Magalhães, Bukayo Saka na Leandro Trossard aliyetokea benchi.

Ni mara ya kwanza kwa Arsenal kufunga mabao matano katika mechi ya ugenini ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu Oktoba 2008.

Arteta alichukua mikoba ya Arsenal Desemba 2019 na kuwarudisha kwenye mashindano ya Ulaya baada ya kukosekana kwa miaka sita.

Alipoulizwa kama huu ulikuwa ushindi bora wa Arsenal ugenini chini ya usimamizi wake, Arteta alijibu: „Kwa hakika, hasa dhidi ya mpinzani tuliyecheza nyumbani kwao.

"Sidhani kama wamepoteza hapa kwa muda wa miezi 18. Wamekuwa katika hali ya juu, wamekuwa bora zaidi kuliko kila mtu ambaye wamecheza hapa.

"Kwa hakika ni ushindi wa kihistoria kwa sababu matokeo yalikuwapo mara chache tulipocheza na timu kubwa. Tulicheza na Paris Saint-Germain na tulikuwa wa kipekee tena. Tulicheza na Bayern Munich na tulikuwa wa kipekee.

"Lakini tulifanya makosa fulani na yalitugharimu. Hicho ndicho kiwango. Inabidi tuweze kustahimili. Ni lazima ufanye hivyo. Hiyo inajenga imani. Tunahitaji uthabiti huo kwa sababu uwezo upo."

Matokeo hayo yanaifanya Arsenal kufikisha pointi 10 baada ya michezo mitano, ndani ya 8-bora kabla ya mechi za Jumatano na mechi inayofuata dhidi ya AS Monaco mnamo Desemba 11 huko Emirates.

# Guardiola afunguka wana wakati mgumu

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema Manchester City wako katika msimu "mgumu" baada ya kulazimishwa sare ya mabao 3-3 na Feyenoord kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi.

Wakiwa wametoka kupokea vichapo vitano mfululizo, Manchester City walipoteza uongozi wa mabao matatu kwa moja katika dakika 15 za mwisho na kutoka sare katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad.

Katika hatua moja, City ilikuwa kwenye nafasi ya tano kwenye jedwali la Ligi ya Mabingwa, lakini sasa ipo nafasi ya 15.

"Utakuwa msimu mgumu kwetu na tunapaswa kuukubali kwa hali nyingi," alisema Guardiola.

"Leo (juzi) kwa bahati mbaya mchezo ulifanyika vizuri na hatukuwaadhibu kwa wakati sahihi, timu ilijituma sana katika mambo mengi lakini kwa bahati mbaya kwa sasa kuna kitu kinatokea na hatuna nguvu za kutosha, inabidi tujaribu kuepukana na makosa hayo."


City walionekana kujiandaa kupata ushindi mzuri kwa mabao mawili kutoka kwa Erling Haaland na lingine kutoka kwa Ilkay Gündogan.

Kilichofuata ni kuanguka kusikoweza kuelezeka wakati timu ya Guardiola iliporuhusu mabao matatu ya dakika za mwisho.

"Haikuwa lazima kuwaambia chochote, wanalijua kabisa," alisema bosi huyo wa City.

"Ni jinsi ilivyo, ngumu kumeza hivi sasa. Mchezo ulikuwa mzuri, tulicheza vizuri, tulifunga mabao matatu na tungeweza kufunga zaidi. Sio juu ya kutokimbia au kutojitolea."

City watacheza na Liverpool kwenye Ligi Kuu England itakayofanyika Jumapili na Guardiola anakabiliwa na kazi ya kujaribu kuwainua wachezaji wake baada ya matokeo mabaya.



# KOMPANY: SIELEWI MUUNDO WA UEFA

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Vincent Kompany, amesema haelewi kikamilifu namna muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya unavyofanya kazi baada ya timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain katika mechi iliyochezwa juzi usiku.

Bayern Munich ilihitaji bao la kipindi cha kwanza kutoka kwa beki, Kim Min-Jae, ili kupambana na wachezaji 10 wa PSG na kupata ushindi wa tatu katika mechi tano walizocheza.

"Siangalii jedwali kwa sababu, kusema ukweli. Bado sielewi," alisema Kompany akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo. „Itaonekana vizuri ikiwa tutashinda mechi chache zaidi."

Bavaria hao walipanda hadi nafasi ya 11 wakiwa na pointi tisa kutokana na michezo mitano, pointi moja kutoka nafasi nane za juu zinakufanya ufuzu moja kwa moja kwa hatua ya 16 bora.

PSG wako nafasi ya 26 wakiwa nje ya mchujo huku mechi tatu zikisalia katika awamu ya kwanza.

Katika muundo mpya wa ligi ya timu 36 msimu huu, timu hukutana na timu nane tofauti badala ya kukutana na wapinzani watatu mara mbili.

Timu nane bora zinatinga moja kwa moja hatua ya 16 bora, huku zile zinazomaliza katika nafasi ya tisa hadi 24 zikiingia hatua ya mtoano kwa mikondo miwili ili kupata nafasi ya kutinga katika hatua inayofuata.

"Kilicho muhimu ni kufikia lengo letu. Ikiwa tutashinda michezo yetu iliyobakia tuna nafasi ya kuingia katika nafasi ya nane bora," alisema Kompany ambaye huu ni msimu wake wa kwanza kuinoa Bayern.

"Ninafuraha, uchezaji wetu katika kipindi cha kwanza ulikuwa mzuri sana, nidhamu ilikuwapo, tungeweza kufunga bao moja au mawili zaidi, lakini matokeo ni mazuri.

„Tuko katika njia sahihi, lakini tunafanya kazi ili kuwa bora zaidi."

# AZAM YATAMBA KUICHAPA SINGIDA BS ILIYOJIIMARISHA

**Na Somoe Ng'itu**

VITA ya kuwania pointi tatu muhimu inatarajiwa kuendelea leo kwa wenyeji Azam FC kuwakaribisha Singida Black Stars katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Azam na Singida Black Stars zitakutana kila moja ikiwa na pointi 24 kibindoni baada ya kucheza michezo 11 sawa na vinara Simba yenye pointi 28.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na wanaamini wataingia kupambana kuhakikisha wanapata ushindi.

Taoussi alisema wamejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu wapinzani wao wamekuwa na kiwango bora na wanarekodi nzuri katika michezo iliyotangulia.

"Tuko tayari kwa ajili ya mechi hii, tunaendelea kupambana kuhakikisha tunapata ushindi, malengo yetu ni kutwaa ubingwa na kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwakani," alisema kocha huyo.

Kaimu Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Ramadhani Nsanzurwimo, alisema wamejipanga kucheza soka la ushindani kwa sababu wanakutana na timu yenye wachezaji ‚wakubwa' na wenye uzoefu katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nsanzurwimo alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na malengo yao ni kupata ushindi na si matokeo mengine.

"Tunajua mechi itakuwa ngumu, Azam wanataka kwenda juu na sisi tunataka kubaki hapo hapo, tunatarajia watu watashuhudia mechi nzuri na yenye ushindani, ni mechi kubwa, lengo letu ni kupata pointi tatu muhimu," alisema Nsanzurwimo.

Aliongeza hakuna mechi rahisi katika Ligi Kuu msimu huu kwa sababu timu zote zimejiimarisha kupata matokeo chanya na si kusindikiza wengine.

"Kila siku tunapokutana na Azam inakuwa ni mechi nzuri na mechi ya kupendeza. Wao wana timu nzuri na sisi tunatimu nzuri, hatujaja kutembea hapa Dar es Salaam, tumekuja kutafuta pointi tatu," alisema kocha huyo.

Alisema pia kikosi chake hakijatetereka kutokana na kutimuliwa kwa aliyekuwa Kocha Mkuu, Patrick Aussems, kwa sababu yeye (Nsanzurwimo) na wengine walikuwapo katika benchi la ufundi, hivyo wataendeleza mazuri yaliyopo.

Naye nyota wa Singida Black Stars, Ayubu Lyanga, alisema wamejiandaa vizuri kuondoka na ushindi katika mechi hiyo na yaliyotokea katika mchezo uliopita yameshaondoka kwenye akili zao.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena kesho kwa KMC kuwaalika Tabora United wakati Fountain Gate itacheza dhidi ya JKT Tanzania na keshokutwa Namungo itawakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi.

# Makocha, waamuzi kunolewa Ruangwa

**Na Mwandishi Wetu, RUANGWA**

WAZIRI Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Kassim Majaliwa, amesema atapeleka wakufunzi wa kuwanoa makocha wa timu za mpira wa miguu zilizoko katika jimbo hilo.

Majaliwa alisema hayo wakati akishuhudia mechi ya fainali ya Kombe la Jimbo (Jimbo Cup), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ambapo Stand FC ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Kiongozi huyo alisema mashindano hayo yanatumika kuboresha maendeleo ya mpira wa miguu katika wilaya hiyo.

"Nitazungumza na Chama cha Makocha Taifa ili watupatie wakufunzi ambao watakuja kutoa mafunzo makocha wa Wilaya ya Ruangwa ya namna bora ya kusimamia timu zetu," alisema Majaliwa.

Aliongeza Ruangwa imeamua kujizatiti katika mpira wa miguu na kusema ni muhimu kuwa na waamuzi wenye uwezo mkubwa wa kusimamia michezo.

"Chama cha Mpira cha Wilaya orodhesheni marefa waliopo katika wilaya hii, nitaomba uongozi wa marefa tupate kiongozi mmoja ili aje aendeshe semina kwa marefa wetu," aliongeza.

Katika hatua nyingine Majaliwa alisema mashindano hayo yatasaidia kuongeza nguvu katika kikosi cha Namungo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa kati wa Al Hilal ya Sudan, Khadim Diaw, katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ililala mabao 2-0. **PICHA: YANGA SC**

# TZ Prisons kusajili hawa dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufungwa bao 1-0 na JKT Tanzania, Kocha Mkuu wa Prisons, Mbwana Makata, amesema anatarajia kusajili wachezaji wazoefu na Ligi Kuu Tanzania Bara wakati wa dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa.

Makata aliliambia gazeti hili anaamini kukosekana kwa wachezaji wazoefu ndio jambo linalowatesa kwa sasa.

Kocha huyo alisema timu yake inaundwa na idadi kubwa ya wachezaji wengi, ambao pamoja na kuwa na vipaji, lakini wanakosa uzoefu na ufanisi.

Alisema kukosekana kwa nyota wake wazoefu akiwamo Samson Mbangula, Nurdin Chona na wengine ambao ni majeruhi kunawaathiri katika vita ya kusaka ushindi.

"Kuwakosa wachezaji kama Mbangula, Chona nayo ni moja ya sababu ya kupoteza siyo mechi hii iliyopita, hata nyingine tulizocheza huko nyuma, kwa sababu ni wachezaji wazoefu, tunawaowatumia sasa wengi ni chipukizi, wana vipaji lakini ufanisi wao ni mdogo kutokana na kukosa uzoefu.

Nadhani tunaangalia dirisha dogo ili tusajili baadhi ya wachezaji wazoefu kidogo na Ligi Kuu ili waje wasaidiane na hawa vijana waliopo," alisema kocha huyo.

Aliongeza amebaini tatizo lingine katika timu yake ni kuruhusu mabao ya mapema ambayo yamekuwa kama ugonjwa kwenye kikosi chake.

"Kuna vitu nimeviona, tumefungwa bao la mapema, hii ni mechi ya tatu sasa tunaruhusu kufungwa dakika za mwanzo na tumeshindwa kutumia nafasi tulizozipata, kazi yangu iliyopo ni kuinoa safu ya ushambuliaji kwa kipindi hiki kabla ya dirisha dogo," alisema.

Kwa sasa Prisons inakamata nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 10 kwa michezo 11 iliyocheza, ikishinda miwili, sare nne na kufungwa mitano.

Takwimu zinaonyesha timu hiyo haijashinda mechi yoyote ugenini wala kufunga bao katika michezo mitano iliyochezwa, ikitoka sare tatu na kupoteza miwili.

Michezo

Alhamisi Novemba 28, 2024

Nipashe

## Lewandowski awafikia Ronaldo, Messi Ulaya

UKURASA 21





# SIMBA YATAKATA AFRIKA

Beki wa Simba, Shomary Kapombe (kushoto), akipambana kumiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Bravos do Maquis, Luis Goncalves, kutoka Angola katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

### Kipa Camara shujaa, adaka penalti na kuwanyima Bravos bao la...

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na kiungo mshambuliaji wa kimataifa raia wa Ivory Coast, Jean Ahoua, liliipa Simba ushindi wa kwanza katika mechi ya raundi ya kwanza ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

Ahoua alifunga bao hilo dakika ya 26 kwa penalti baada ya beki wa Bravos do Maquis, Reuben Aderito, kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari wakati akijaribu kuokoa shambulizi kuelekea langoni kwao.

Awali krosi iliyopigwa na Ladack Chasambi, ilikuwa inakwenda katika kichwa cha Kibu Denis dakika ya 25, lakini beki huyo aliokoa na mkono ili usimfikie winga wa Simba ambaye alikuwa amesharuka kichwa cha kuchumpa na mwamuzi, Ibrahim Mutaz kutoka Libya akaamuru pigo la penalti.

Ahoua aliukwamisha wavuni na bao hilo likasimama hadi mwamuzi huyo alipopuliza filimbi ya mwisho kuashiria dakika 90 za mchezo huo zimemalizika kwa wenyeji kuondoka na pointi tatu muhimu.

Hata hivyo haukuwa ushindi rahisi kwa sababu dakika moja baada ya mapumziko, Bravo do Maquis, pia walipata penalti, baada ya Kibu kumkwatua, Emmanuel Edmond, akiwa katika harakati za kutaka kuuokoa.

Shujaa alikuwa ni kipa wa Msimbazi, Moussa Camara, alipofanikiwa kupangua penalti ya Edmond ambaye yeye mwenyewe alichukua jukumu la kupiga.

Camara alifanikiwa kuliweka salama lango la Simba alipookoa michomo mingi ya hatari kutoka kwa mastraika wa Bravos do Maquis.

Hatari kubwa zaidi ilikuwa ni dakika ya 58, wakati Edmond alipobaki na kipa huyo akapiga shuti ambalo alilipangua, mpira ukaenda kwa Keoikantese Abednego, lakini alijitoa mzima mzima na kuokoa kwa mara ya pili mfululizo hali iliyosababisha aumie na kuomba msaada wa matibabu.

Katika mchezo huo, kila timu ilitawala kipindi kimoja, Simba ikitakata kipindi cha kwanza huku Bravos do Maquis wakifunguka kipindi cha pili kwa pasi za kuonana na kupiga mpira mirefu iliyoleta hatari zaidi langoni mwa wenyeji.

Simba ilifanya shambulio la kwanza katika lango la Bravo do Maquis, dakika ya sita, ambapo gonga za Ahoua na Chasambi zilimkuta Kibu akiwa katika nafasi nzuri, lakini akapiga nje.

Simba ilirejea tena langoni mwa wageni wao dakika mbili baadaye, lakini shuti la Mganda, Steve Mukwala, akiwa nje ya eneo la 18 lilitoka nje.

Kibu angeweza kuipatia Simba bao dakika ya 15, lakini shuti lake dhaifu liliishia mikononi kwa kipa, Landu Mavanga.

Simba iliendelea kukosa mabao, Mukwala kwa mara nyingine, akiwa amemzidi nguvu na mbio beki, Samuel Bengue, akiwa peke yake na Mavanga alipiga nje huku mashabiki wakiwa wameshanyanyuka kujiandaa kushangilia.

Kipindi cha kwanza, Bravo do Maquis mara nyingi walikaa nyuma na mpaka dakika 45 zinamalizika hawakufanya shambulio lolote la maana, kabla ya kubadilika kipindi cha pili.

Timu zote zilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Augustine Okejepha, Kibu, Ahoua, Mukwala na Chasambi, wakiingia, Debora Fernandes, Joshua Mutale, Leonel Ateba, Edwin Balua na Mzamiru Yassin, lakini matokeo hayakubadilika, badala yake timu zote zilishambulia kwa zamu na kukosa mabao.

Mechi nyingine ya Kundi A kati ya CS Sfaxien ya Tunisia na CS Costantine ya Algeria, ilitarajiwa kuchezwa jana usiku jijini Tunis.

## Ramovic: Wachezaji wangu hawako fiti

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukaribishwa na kichapo, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema timu yake ilipoteza mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan kwa sababu wachezaji wake walikosa utimamu wa mwili na pumzi ya kutosha kumudu kucheza dakika zote 90.

Yanga ilipoteza mechi hiyo kwa kufungwa mabao 2-0, mchezo wa Kundi A uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Ramovic, alisema tatizo aliloliona katika kikosi chake ni wachezaji kutomudu kucheza kwa nguvu inayofanana, hivyo itachukua muda ‚kidogo' kurekebisha mapungufu hayo na si jambo linalotatulika kwa haraka.

"Tatizo kubwa linalowakabili wachezaji wangu ni kukosa utimamu wa mwili na pumzi, hivyo wanachoka mapema hawawezi kumaliza dakika 90 kwa nguvu na kasi ile ile, na hili linatatulika kwa kunipa muda, japo siwezi kusema nitalitibu kwa muda gani, labda wiki tatu au zaidi nitaweza kulitatua," alisema Ramovic.

Kocha huyo alisema kipindi cha kwanza timu yake ilitawala mchezo wakapata nafasi za kufunga na endapo wangefanikiwa kupata mabao, hadhithi ingekuwa nyingine.

"Kipindi cha kwanza tulitawala mpira tukapata nafasi lakini hatukufunga, kuna nafasi ilitokea kama Stephane Aziz Ki angefunga, ingewezekana mambo yangekuwa tofauti.

Hata hivyo, tuna michezo mitano imebaki, safari bado ni ndefu katika kundi hili, tunakwenda kufanyia kazi mapungufu ili tushinde michezo inayokuja," Ramovic alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, amefurahishwa na ushindi huo wa ugenini, ingawa alisema haukuwa ushindi rahisi kutokana na ubora wa Yanga.

"Hatukuanza mchezo vizuri, hatukuwa tunamiliki mpira, tulikuwa tunapoteza mipira mingi, nafikiri mwanzoni walipata nafasi mbili za uwezekano wa kufunga lakini baada ya hapo tukamudu kuzuia, baadaye tukafunga mabao mawili yaliyokuwa muhimu kwetu.

Niliwaambia viungo na mabeki wangu wasiwape sana nafasi ya kukaa na mpira na wasikae nao mbali sana na hilo lilisaidia sana kwa sababu wachezaji wao kabla hajafikiria nini cha kufanya, vijana wangu tayari walikuwa wameshafika na kutibua mipango," Ibenge alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >